**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**AFISI YA RAIS - KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI - AFISI YA RAIS - KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

**MWL. HAROUN ALI SULEIMAN (MBM)**

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

**MEI, 2023**

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati, ili liweze kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kwa Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora - Zanzibar.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, kwa kutuwezesha kukutana leo hii tukiwa na afya njema, amani na utulivu. Aidha, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu yanayochangia katika kujenga ustawi wa wananchi wa Zanzibar na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

3. **Mheshimiwa Spika,** naomba nimpongeze tena Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuendelea kuiongoza Zanzibar kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta za kiuchumi na kijamii na katika kustawisha demokrasia, kuzingatia misingi ya utawala bora, kuendelea mapambano dhidi ya rushwa na

kuheshimu haki za binaadamu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe nguvu na afya njema ili tuendelee kufaidika na matunda ya jitihada na mapenzi yake kwa wananchi wa Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Makamo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa upande wa Zanzibar. Namuahidi kwamba tutashirikiana nae bega kwa bega katika kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020-2025 na kutimiza ahadi alizozitoa kwa wananchi wakati wa Uchaguzi Mkuu. Aidha, nampongeza kwa dhati Ndugu Mohamed Said Mohamed (Dimwa) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM – Zanzibar na kumuahidi mashirikiano ya hali ya juu pamoja katika utekelezaji wa majukumu yake.

5. **Mheshimiwa Spika,** nikiwa Waziri ninaesimamia masuala ya Utumishi wa Umma hapa Zanzibar, kwa niaba ya Watumishi wa Umma nachukua fursa hii kumpongeza na kumshukuru kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa marekebisho makubwa aliyoyafanya ya kupandisha mishahara ya watumishi wa umma na kuruhusu kuanza kutumika kwa

Miundo ya Utumishi ambayo inazingatia sifa za kielimu na uzowefu wa mtumishi. Utekelezaji wa Miundo ya Utumishi umeondoa malalamiko ya muda mrefu ya Watumishi wa Umma ambapo kwa utaratibu wa zamani uzoefu wao haukuwa ukizingatiwa katika kurekebisha maslahi yao. Niwaombe Watumishi wa Umma wote, wathamini juhudi hizi za Mheshimiwa Rais na waongeze ari na juhudi katika kutekeleza majukumu yao.

6. **Mheshimiwa Spika,** nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamo wa Kwanza wa Rais, kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuiongoza Zanzibar. Vile vile, tunamshukuru kwa miongozo na maelekezo yake anayoyatoa ambayo yanatusaidia sana katika kusimamia haki na utumishi wa umma.

7. **Mheshimiwa Spika,** pongezi zangu za dhati ziende kwa Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais, kwa kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali katika Baraza lako Tukufu na kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa Ilani ya CCM hapa Zanzibar pamoja na majukumu mbali mbali kwa manufaa ya Wananchi wa Zanzibar. Usimamizi wake wa karibu umekuwa chachu katika kuimarika kwa utendaji katika Taasisi za Umma.

8. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa kuliongoza kwa umakini na umahiri Baraza hili Tukufu katika kufikia maamuzi mbali mbali yenye manufaa kwa ustawi wa jamii ya Wazanzibari na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Juhudi zenu tunazithamini sana.

9. **Mheshimiwa Spika,** shukurani zangu maalum ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Machano Othman Said, Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Mfenesini na Makamo Mwenyekiti Mtumwa Peya Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Bumbwini, kwa ushauri na miongozo waliyotupa katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023. Aidha, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano waliotupa katika matayarisho ya bajeti ya Afisi yangu kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Napenda kuihakikishia Kamati na Baraza lako Tukufu kwamba maoni na mapendekezo yaliyotolewa yamezingatiwa na kufanyiwa kazi katika Bajeti hii.

10. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue fursa hii pia kuwashukuru Mawaziri wenzangu na wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kwa ushirikiano mnaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Ni dhahiri kwamba mashirikano baina yetu ni nguzo muhimu katika

kufanikisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM, mipango na mikakati ya kitaifa katika kuleta maendeleo na kukuza uchumi na hali za maisha ya wananchi wa Zanzibar.

11. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, napenda kuipongeza kwa dhati na kuishukuru familia yangu hasa mke wangu mpendwa na watoto wangu wote kwa msaada wao mkubwa kwangu na mashirikiano yao yanayonipa nguvu ya utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, kwa namna ya kipekee nawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Makunduchi kwa upendo walionao kwangu na ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Nathamini sana ustahamilivu walionao kwangu, hata pale ambapo ninapokuwa nimebanwa na majukumu ya kitaifa nje ya Jimbo langu la uchaguzi wao wanakuwa mstari wa mbele kuniunga mkono.

    Mimi nawapenda sana, na ahadi yangu kwao ni kwamba niko pamoja nao na katu sitowaangusha. Aidha, nakishukuru sana Chama changu Chama Cha Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini na ahidi utekelezaji uliotukuka wa Ilani yetu ya Uchaguzi ya CCM.

12. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo sasa naomba kuwasilisha Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2022/2023 na Mwelekeo wa Bajeti ya Mwaka 2023/2024 kama ifuatavyo:

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

13. **Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ilitekelezwa kwa kuzingatia Mipango na Miongozo ya kitaifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 pamoja na Mpango wake wa Utekeleza 2021-2026, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020/2025, Mpango wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma awamu ya pili, Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Sheria awamu ya pili, Sera na Sheria mbali mbali zinazoongoza Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu. Aidha, utekelezaji umezingatia maelekezo mbali mbali aliyoyatoa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ikiwa ni pamoja na maagizo aliyoyatoa katika Hotuba yake ya tarehe 11 Novemba 2020 wakati alipozindua Baraza la Kumi la Wawakilishi.

14. **Mheshimiwa Spika** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara yangu imesimamia jumla ya mafungu 13 ya Bajeti yaliyotekelezwa kupitia Programu kuu 16 ambazo zinatekelezwa na Idara na Taasisi zinazojitgemea zilizo chini ya Wizara. Programu hizo ni kama ifuatavyo: i) Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria; ii) Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora; iii) Programu ya Uratibu na Uendeshaji wa ARKSUUB; iv) Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa

Umma; Programu hizi zimo katika fungu **G01**; na v) Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki **G02**; vi) Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria **G03**; vii) Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai **G04**, viii) Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria **G05**; ix) Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini **G12**; x) Programu ya Huduma za Serikali Mtandao **G13**; xi) Programu ya Usimamizi wa Masula ya Dini **G14**; Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi wa Umma **G15**; xii) Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma **E04**; xiii) Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi **E05**; xiv) Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma **E07**; na xv) Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini **E08**. Vile vile, Afisi hii imesimamia ruzuku ya Chuo Cha Utawala wa Umma pamoja na Skuli ya Sheria Zanzibar.

15. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha **2022/2023**, ilipanga kutumia jumla ya Shilingi **49,662,665,000**, ambapo kati ya hizo, Shilingi **44,328,660,000** zilipangwa kutumika kwa matumizi ya kazi za kawaida na mishahara na Shilingi **3,261,405,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi **2,072,600,000** ni ruzuku kwa Taasisi zinazopokea ruzuku kutoka Serikalini.

16. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi **2023**, jumla ya Shilingi **31,145,457,454** zimepatikana, sawa na asilimia 68 ya lengo ambapo Shilingi **22,504,174,664** zilitumika kwa malipo ya mishahara na Shilingi **8,641,282,790** zilitumika kwa matumizi mengineyo na ruzuku kwa ajili ya Chuo Cha Utawala wa Umma na Skuli ya Sheria. Kwa upande wa mapato, Ofisi ilikusanya jumla ya Shilingi **1,401,480,604** kupitia vyanzo vya mapato yake **(Kiambatanisho nam. 1a & 1c)**

    Taarifa za makadirio ya fedha na matumizi halisi kwa kila fungu na programu zilizomo katika Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora zitaonekana katika mafungu ya taasisi hizo kupitia program husika.

17. **Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuanza kuelezea utekelezaji wa Programu moja moja zilizo chini ya Wizara yangu, naomba nielezee mafanikio ya jumla yaliyopatikana kama ifuatavyo:-

    i. Wizara imefanikiwa kufanya marekebisho ya mishahara na stahiki nyengine za watumishi kwa ufanisi na uwazi. Jumla ya Watumishi wa Umma 55,232 wamefaidika na marekebisho hayo. Aidha, Miongozo na Matoleo 32 yanayofafanua taratibu za malipo na stahiki za watumishi wa umma na masuala mengine ya kiutumishi yametolewa na yameanza kutumika ;

ii. Kuongezeka kwa matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika utowaji wa huduma mbali mbali. Mifumo hiyo ni pamoja na: Mfumo wa Ofisi Mtandao ***(e-Office)*** ambao unatumika na zaidia ya asilimi 60 ya Taasisi za Umma; Mfumo wa Maombi ya Ajira (Zan-Ajira); Mfumo wa Taarifa za Watumishi na Malipo ***(Human Resource and Payroll Management Information System- HR-PAYMIS)***; Mfumo wa Usajili na Usimamizi wa Mawakili **(E-Wakili)**; Mfumo wa Usimamizi wa Kesi ***(Case Management System);*** Mfumo wa Kieletroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni; Mfumo wa Usimamizi wa Mirathi ***(Islamic Inheritance Management System);*** Maktaba Mtandao ***(e-library)*** ya Skuli ya Sheria. Mifumo hii ipo katika hatua mbali mbali za maendeleo, baadhi imeanza kutumika na baadhi imo katika hatua za mwisho za matayarisho;

iii. Kuongezeka kwa uwezo wa kitaaluma wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hali iliyopelekea kualikwa kufanya ukaguzi na makampuni binafsi pamoja na Ofisi za Ubalozi wa Tanzania nje ya nchi;

iv. Kukamilika kwa Mpango Mkakati wa Mageuzi wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Mpango huu unatarajiwa kuleta

mageuzi makubwa katika utendaji kazi na utowaji wa huduma;

v. Kuongezeka kwa wigo wa upatikanaji wa Msaada wa Sheria, kwa kuongezeka kwa idadi ya watoaji wa msaada wa kisheria katika jamii na kufikia 230 na kuna Taasisi 17 zinazojishughulisha na utowaji wa msaada wa kisheria. Aidha, hivi sasa wananchi wanaweza kupata muongozo juu ya upatikanaji wa msaada wa kisheria kupitia Masheha wa maeneo yao.

***G01-Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora***

18. **Mheshimiwa Spika,** Fungu G01 linahusisha Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria; Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora; Programu ya Uratibu na Uendeshaji wa OR-KSUUB na Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi.

***Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria***

19. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Programu hii unasimamiwa na Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria na katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Idara ilitekeleza kazi zifuatazo:-

i. Vipindi 20 vya elimu kwa umma juu ya masuala ya sheria (Unguja 12 na Pemba 8) viliandaliwa na kurushwa hewani kupitia Redio na Televisheni za Umma na Binafsi;

ii. Kuendesha Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia pamoja na wahusika wa msaada wa kisheria juu ya kuitambulisha Kampeni hiyo kwa Unguja na Pemba ambapo jumla ya washiriki 60 wakiwemo wanawake 25 wanaume 35 walihudhuria;

iii. Maadhimisho ya tatu ya Wiki ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2022 yaliadhimishwa ambapo mkutano wa kilele cha wiki hiyo ulifanyika katika Ukumbi wa Sheikh Idris Abdul Wakil. Kazi nyengine zilizofanyika katika kuadhimisha wiki hiyo ni pamoja na mikutano na waandishi wa habari, kutembelea wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo na mahabusu na wanafunzi 154 waliopo katika Vyuo vya Mafunzo kwa Unguja na Pemba walipatiwa huduma za msaada wa kisheria; kambi za utoaji msaada wa kisheria na kona ya msaada wa kisheria ziliweka katika shehia na wanajamii walipatiwa elimu na misaada ya kisheria na wananchi 328 wakiwemo wanawake 135 na wanaume 193 walipatiwa huduma hiyo.

iv. Mafunzo ya siku mbili (2) kwa wahanga 60 wa masuala ya udhalilishaji (wanawake 48 na wanaume 12) yalitolewa kuhusiana na kuwaongoza wahanga hao katika kutoa ushahidi na kuwajenga kisaikolojia kukabiliana na hali halisi na matukio yaliyowakuta.

v. Malalamiko 11 yalipokelewa na wahusika walipatiwa msaada wa kisheria. Malalamiko hayo yanahusiana na mgogoro wa ardhi 2, udhalilishaji 2, malipo ya deni 1, ulezi wa watoto 1, mgawanyo wa mali baada ya kuachana 1, migogoro inayohusiana na duka 2 wa mlango wa duka 2, na madai ya mzazi kwa mwalimu wa skuli mmoja;

vi. Madrasa za Qur-an 16 (8 Unguja na 8 Pemba) walipatiwa mafunzo juu ya kujilinda na masuala ya udhalilishaji, wanafunzi 2,365 (wanawake 1,169 na wanaume 1,196) walifaidika na mafunzo hayo.

**20. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria imeanza kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia ambayo inatekelezwa Tanzania nzima. Kwa upande wa Zanzibar, mikutano ya kuitambulisha Kampeni hiyo ilifanyika kwa wahusika wa msaada wa kisheria Unguja na Pemba na washiriki 60 (wanawake 25 wanaume 35) walihudhuria.

21. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Programu hii ilipangiwa Shilingi **283,240,000**, hadi kufikia Machi **2023**, Shilingi **153,218,514** zimepatikana (sawa na asilimi 54) ambapo Shilingi **78,515,860** zilitumika kwa mishahara na Shilingi **74,702,654** zilitumika kwa kutekeleza kazi za Idara. Aidha, Idara pia ilipata Shilingi **68,000,000** kutoka kwa Wahisani wa Maendeleo kupitia Mradi wa LSF wa Kuimarisha Upatikanaji wa Haki Zanzibar (Kiambatanisho nam. 1a).

***Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora***

22. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Idara ya Utawala Bora na kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

   i. Sera ya Utawala Bora ya Mwaka 2011 imefanyiwa mapitio na rasimu ya kwanza imekamilika kwa kuwasilishwa Serikalini. Idara pia imekamilisha Rasimu ya Mswada wa Sheria ya Majukumu ya Kijamii (Corporate Social Responsibility) na rasimu hiyo ipo katika hatua ya kuiwasilisha Serikalini;

   ii. Idara imeshiriki katika Maonesho ya Tisa ya Biashara yaliofanyika Zanzibar na iliweza kuwapatia wananchi 205 elimu na uelewa

juu ya Utawala Bora, aidha, Idara pia ilishiriki katika Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu yaliyofanyika Zanzibar mwezi Desemba 2022;

iii. Elimu ya utawala bora imetolewa kwa jamii kupitia mikutano 21 iliyofanyika katika ya ngazi ya shehia na vipindi 53 vya Radio na TV. Masheha, wanajamii na wanachi kwa ujumla walielimishwa juu ya dhana ya utawala bora, uzalendo, vita dhidi ya masuala ya udhalilishaji, kudumisha amani na utulivu pamoja na ushirikishwaji wananchi katika shughuli za Serikali.

**23. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilipangiwa Shilingi **306,353,000.** Hadi kufikia mwezi Machi **2023**, Shilingi **200,264,391** zimepatikana sawa na asilimia **65** ya lengo. Kati ya fedha zilizopatikana, Shilingi **164,853,000** zilitumika kwa mishahara na Shilingi **50,202,621** zilitumika kwa kazi za uendeshaji **(Kiambatanisho nam. 1a).**

Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora

**24. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2023, kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

i. Mpango wa Rasilimali Watu wa Miaka Mitano (2023/2024 hadi 2027/2028)

ambao umezingatia utoaji wa nyongeza za mshahara, upandishwaji wa vyeo na mafunzo kwa watumishi imetayarishwa kwa Wizara na Taasisi zote za Umma;

ii. Watumishi 29 wamepatiwa mafunzo ambapo watumishi wanne wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu, watumishi 22 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi yakiwemo mafunzo ya Udereva wa Viongozi, Utunzaji wa Kumbukumbu, usalama wa mtandao na watumishi 3 wamepatiwa Mafunzo Elekezi;

iii. Watumishi 188 wamepatiwa stahiki mbalimbali za kiutumishi ikiwa ni pamoja na posho la likizo, posho nyeti na malipo ya muda wa ziada wa saa za kazi; na

iv. Habari na machapisho yapatayo 110 yanayohusu Wizara na Taasisi zake yamechapishwa na kusambazwa kupita vyombo vya habari na tovuti ya Wizara. Aidha, malalamiko 158 yaliyowasilishwa kupitia mfumo wa Sema na Rais Mwinyi yamepatiwa ufumbuzi.

25. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, programu hii ilipangiwa kutumia Shilingi **2,585,374,000** kwa mishahara na matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi **2023,** fedha zilizopatikana ni Shilingi **2,253,006,625**

sawa na asilimia **87** ya lengo na kati ya fedha zilizopatikana Shilingi **1,207,628,180** zilitumika kwa mishahara na Shilingi **1,045,378,445** kwa ajili ya matumizi mengineyo **(Kiambatanisho nam. 1a).**

**26. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2023, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imetekeleza kazi zifuatazo:

i. Ripoti mbali mbali za utekelezaji zimetayarishwa na Idara imeratibu vikao mbali mbali vya Wizara;

ii. Mapitio na marekebisho ya Sheria nne yamefanyika. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Sheria ya Wakala wa Serikali Mtandao, Sheria ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi na Sheria ya Chuo cha Utawala wa Umma (IPA). Kati ya sheria hizo, Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi na Sheria ya Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) tayari zimewasilishwa katika Baraza hili Tukufu;

iii. Idara kwa kushirikiana Benki ya Dunia imetayarisha utafiti kuhusu Uimarishaji wa Utumishi wa Umma Zanzibar “The diagnostic study to enhance public service

governance in Zanzibar" na ripoti yake tayari imeshawasilishwa Serikalini kupitia Kamati ya Makatibu Wakuu;

iv. Vilevile, Idara kwa kushirikiana na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana pamoja na Chuo Cha Utawala wa Umma imeendelea na matayarisho ya kufanya utafiti kuhusu "Sababu Zinazopelekea Watu Kuchelewa Kurithi na Athari Zake katika Jamii Zanzibar."

27. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha **2022/2023,** Programu hii ilipangiwa Shilingi **363,010,000** kwa mishahara na matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi **2023,** fedha zilizopatikana ni Shilingi **189,089,305** sawa na asilimia **52** ya lengo. Kati ya fedha zilizopatikana, Shilingi **126,511,150** zilitumika kwa ajili ya mishahara na Shilingi **62,578,155** kwa matumizi mengineyo **(Kiambatanisho nam. 1a).**

***Uratibu wa Usimamizi wa Programu za Miradi ya Wizara***

28. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini ya Wizara, imeratibu na kusimamia utekelezaji wa programu za miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:

***Mradi wa Uwezeshaji wa Kisheria na Upatikanaji wa Haki Awamu ya Pili (LEAP II).***

**29.** **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ni wa miaka mitatu (2022–2026) na utekelezaji wake ulianza mwezi Oktoba 2022 kupitia ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP). Taasisi zinazotekeleza mradi huu ni pamoja na Mahkama Kuu, Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Idara ya Msaada wa Kisheria na Chuo Cha Mafunzo. Idara imekamilisha matayarisho wa Mpango wa Utekelezaji na Bajeti kwa mwaka 2023 na tayari umeshawasilishwa UNDP na fedha za utekelezaji wa kazi zilizopangwa zimeshaingizwa katika hesabu (account) ya Wizara.

***Program ya Mradi wa Upatikanaji wa Haki kwa Wanawake na Watoto na Kuzuia Vitendo vya Udhalilishaji***

**30.** **Mheshimiwa Spika,** Idara imeratibu hatua za awali za uanzishwaji wa Mradi wa Upatikanaji wa Haki kwa Wanawake na Watoto na kuzuia Vitendo vya Udhalilishaji kupitia ufadhili wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wanawake (UN Women). Mpango wa Utekelezaji pamoja na bajeti tayari zimeshawasilishwa kwa wahisani.

### *Programu ya Uratibu wa ARKSUUB - Pemba*

31. **Mheshimiwa Spika,** programu ya Uratibu wa ARKSUUB imeratibu na kusimamia shughuli za utawala, utumishi na mipango ya Afisi kwa upande wa Pemba. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2023, Afisi imeweza kusimamia mafunzo ya Maofisa Wadhamini pamoja na kufanya ziara za kutembelea Wizara za Serikali na taasisi zake kwa lengo la kusikiliza changamoto za watumishi na kutoa maelekezo kwa mujibu wa kanuni na Sheria za Utumishi. Vile vile, imepokea maoni kutoka kwa wananchi wa maeneo mbali mbali ya Pemba kuhusu uwajibikaji wa Wizara katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, imetoa elimu kwa jamii kuhusu masuala mbali mbali mtambuka, ikiwemo elimu kuhusu udhalilishaji.

32. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi **572,573,000** kwa mishahara na matumizi mengine. Hadi kufikia Machi **2023,** Shilingi **277,156,680** zimepatikana sawa na asilimia 48 ya lengo . Kati ya fedha zilizopatikana, Shilingi **225,628,870** zimetumika kwa mishahara na Shilingi **51,527,810** zimetumika kwa matumizi mengineyo. **(Kiambatanisho nam. 1a).**

***Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma***

33. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hii, Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu na Maendeleo, imetekeleza kazi zifuatazo katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2023:- 2023/2024 hadi 2027/2028

i. Idara imeratibu utaarishaji wa Mpango wa Miaka Mitano (5) wa Rasilimaliwatu kwa taasisi zote za umma;

ii. Uhakiki wa wafanyakazi umefanyika kwa lengo la kuimarisha utendaji na kuhakikisha matumizi sahihi ya rasilimaliwatu. Kutokana na uhakiki uliofanyika, Wafanyakazi 236 kutoka Wizara na Taasisi mbali mbali wamehamishwa na kupelekwa katika Wizara na Taasisi zenye upungufu wa wafanyakazi kwa mujibu wa taaluma zao;

iii. Idara imeratibu upatikanaji wa fursa za mafunzo ya muda mrefu na mfupi kutoka kwa wadau wa maendeleo. Watumishi 60 wamepata ufadhili wa masomo kupitia ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Serikali ya India, Shirika la Kimataifa la Korea (KOICA) na Shirika la Kimataifa la Japan (JICA). Watumishi 22 ngazi za Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu nchini Korea, Japani na China na

watumishi 38 wameendelezwa kitaaluma kupitia programu ya mafunzo ya muda mfupi nchini India, Korea na Japan;

iv. Idara imesimamia ukamilishwaji wa Mfumo wa Taarifa za Watumishi na Malipo (Human Resource and Pay Roll Management Information System-HR-PAYMIS). Kazi ya kuingiza taarifa za Watumishi katika Mfumo huu imaendelea. Taasisi zote za Umma zitaingiza na kuhakiki Taarifa za Watumishi wao kwa lengo la kupata Taarifa sahihi ili kuiwezesha Serikali kufanya malipo na stahiki mbalimbali za watumishi;

v. Idara imesimamia utoaji wa vibali vya ajira 28 ambavyo vimeridhia nafasi za ajira 2,854. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Serikali imeajiri ajira za kudumu 2,854 pamoja na ajira za Mikataba 438 na kufanya jumla ya ajira zote zilizoajiriwa kufikia 3,292.

34. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** Programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi **472,210,000** kwa mishahara na matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi **2023,** fedha zilizopatikana ni Shilingi **374,032,479** sawa na asilimia **79.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **252,031,587** zimetumika kwa mishahara na Shilingi **122,000,892** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatanisho nam. 1a).**

35. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Miundo ya Taasisis na Maslahi ya Watumishi ambayo nayo kazi zake zinatekelezwa chini ya Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Marekebisho ya mishahara kwa Watumishi wa Umma yamefanyika mwezi Julai, 2022. Marekebisho haya yaliwahusisha watumishi wa Serikali Kuu, Mamlaka na Taasisi za Umma, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Waheshimiwa Madiwani, Watumishi wa Idara Maalum za SMZ, Masheha, watumishi wa Chuo Cha Taifa Zanzibar (SUZA), Watumishi wa vyuo visivyoungana na Chuo Cha Taifa (SUZA), Vyuo vya Mafunzo ya Amali, Maafisa Waandamizi Maalum na Watendaji Wakuu;

ii. Watumishi **16,965** walifanyiwa marekebisho ya Mshahara kutokana na kasoro zilizojitokeza katika marekekebisho ya jumla ya mshahara ya Mwezi Julai, 2022.

iii. Idara iliidhinisha malipo ya malimbikizo ya mshahara kwa awamu ya kwanza kwa watumishi **15,771** ambao mishahara yao ilikosewa wakati wa marekebisho ya jumla. Kazi ya kulipa malimbikizo ya mishahara itaendelea katika mwaka wa fedha 2023/2024;

iv. Idara imekamilisha mapitio ya Miundo ya Wizara 18 za SMZ na sasa Wizara zote za SMZ zina miundo rasmi ya taasisi pamoja na majukumu yao. Aidha, Idara iliratibu zoezi la kuwapanga watumishi wote wa umma katika miundo ya utumishi na kuwekwa katika madaraja na vyeo wanavyostahiki;

v. Idara ilifanya tathmini ya Utekelezaji wa Mikataba ya Utoaji Huduma kwa Umma kwa Wizara mbili na matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kwamba mafunzo zaidi yanahitajika kwa taasisi ili kufanikisha utekelelezaji wa Mikataba hivyo. Idara imepanga kuendesha mafunzo hayo katika mwaka ujao wa fedha 2023/2024;

vi. Idara kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar imefanya ziara ya kubadilishana uzoefu na Ofisi ya Msajili wa Hazina Tanzania Bara kwa lengo la kujifunza pamoja na kubadilishana uzoefu juu ya utaratibu wa uendeshaji na usimamizi wa Taasisi, Mamlaka za umma pamoja na Bodi za Taasisi na Mamlaka hizo. Wizara tayari imewasilisha mapendekezo kuhusu utaratibu wa uendeshaji na usimamizi Serikalini na maamuzi yametolewa kwa lengo la kuongeza ufanisi katika taasisi hizo na Serikali kwa ujumla;

vii. Idara imetoa Miongozo na Matoleo 32 yanayofafanua taratibu za malipo ya stahiki za watumishi wa umma ma masuala mengine ya kiutumishi. Miongozo na matoleo hayo yameanza kutumika;

36. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** programu hii imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi **543,000,000** kwa mishahara na matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi **2023,** Shilingi **482,575,066** zimepatikana sawa na asilimia **89** ya lengo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **380,388,733** zimetumika kwa mishahara na Shilingi **102,186,333** zimetumika kwa matumizi ya mengineyo **(Kiambatanisho nam. 1a).**

***TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU***

37. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imesimamia ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo ya Chuo cha Utawala wa Umma na Skuli ya Sheria kwa ajili ya utekelezaji wa programu za taasisi hizo. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Taasisi hizi zimetekeleza mambo yafuatayo:

***Chuo cha Utawala wa Umma***

38. **Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Utawala wa Umma kimetekeleza yafuatayo:-

i. Kupitia Programu ya Mafunzo ya Muda Mrefu, Chuo kimetoa mafunzo kwa wanafunzi 1,566 (watumishi wa umma 558 na wananchi wa kawaida 1,008) katika ngazi za astashahada, stashahada na shahada katika fani mbali mbali. Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wa umma 902 kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi. Mafunzo hayo yalitolewa kwa Makatibu Muhtasi, Watunza Kumbukumbu, Maafisa Tehama na Viongozi wa Tume ya Kurekebisha Sheria;

ii. Mafunzo elekezi yametolewa kwa Watumishi wapya 2,425 kutoka katika Wizara na Taasisi za Umma Unguja na Pemba;

iii. Katika kuwajengea uwezo wa kitaalamu watumishi wake, Chuo kimewapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi tisa, kati ya hao, wanne katika ngazi ya Uzamili na watano katika ngazi ya Shahada ya kwanza. Vile vile, Chuo kimewapatia mafunzo ya muda mfupi ya kujenga uwezo wa kiutendaji Watumishi tisa;

iv. Tafiti mbili kuhusu "Matumizi na Uendelevu wa Serikali Mtandao katika Taasisi za Umma" na "Sababu za Watumishi Kuhama katika Taasisi za Umma na Athari zitakazo jitokeza katika Utendaji wa Taasisi za Umma." Tafiti

hizo zimeandaliwa na zipo katika hatua ya ukusanyaji wa taarifa kwa upande wa Pemba. Aidha, Chuo kimeendelea kushirikiana na Taaasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi, ikiwemo Chuo cha Utumishi wa Umma Magogoni (TPSC), Chuo Kikuu cha Diplomasia Kurasini (CFR) pamoja na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

39. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023** Chuo kilipangiwa kutumia ruzuku ya Shilingi **1,433,700,000,** kati ya hizo Shilingi **1,380,700,000** kwa matumizi ya mshahara na Shilingi **53,000,000** kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi **2023,** Shilingi **1,170,575,000** zimepatikana sawa na asilimia **82** ya lengo. Aidha, Chuo kilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi **1,630,876,000** kutokana na malipo ya ada za wanafunzi na kimefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi **1,304,869,500** sawa na asilimia **80** ya makadirio.

***Skuli ya Sheria Zanzibar***

40. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi machi 2023, Skuli ya Sheria Zanzibar imetekeleza yafuatayo:-

i. Wanafunzi 21 wamepatiwa mafunzo ya vitendo katika Taasisi za Serikali ikiwemo

Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Mahkama Kuu ya Zanzibar, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na taasisi mbali mbali katika Sekta Binafsi.

ii. Skuli imedahili wanafunzi wapya 101, na wanafunzi 37 wamesajiliwa na wanaendelea na masomo;

iii. Semina za mafunzo ya kubadilishana uzoefu na wakufunzi wa Skuli ya Sheria ya Tanzania (Bara) zimefanyika, na wakufunzi 20 wameshiriki mafunzo hayo. Aidha, wanafunzi 37 wameshiriki kongamano la mafunzo ya sheria kwa vitendo lililofanyika katika Ukumbi wa Mahkama Kuu ya Zanzibar, Tunguu, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini;

iv. Kwa kushirikiana na Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria, Skuli ya Sheria ilisimamia mafunzo elekezi kwa watoa msaada wa kisheria 18 yaliyodhaminiwa na Idara ya Maendeleo ya Kanisa Katoliki, Welezo – Zanzibar.

41. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023** Skuli ya Sheria ilipangiwa kutumia jumala ya Shilingi **529,500,000** kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi **2023,** Shilingi **250,251,000** zimepatikana sawa na asilimia

**47.3** ya lengo. Aidha, Skuli ilipanga kukusanya mapato ya Shilingi **379,000,000,** hadi kufikia Machi **2023** jumla ya Shilingi **44,128,000** zimekusanywa kutokana na malipo ya ada za wanafunzi na mafunzo mafupi ya kujenga uwezo, sawa na asilimia **11** ya makadirio.

## G02: MAHKAMA KUU

***Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki***

42. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya usimamizi na Upatikanaji wa Haki inahusisha kazi za kutafsiri sheria, kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri yote ya jinai na madai yanayowasilishwa Mahkamani. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Mahkama imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Mashauri 13,471 (jinai 10,995 na madai 2,476) yamepokelewa na Mashauri 10,917 kati ya hayo yametolewa uamuzi sawa na asilimia 81. Mashauri 2,554 yanaendelea kufanyiwa kazi;

ii. Kwa upande wa Mahkama Maalum za Udhalilishaji mashauri 359 yamefunguliwa na 174 yametolewa uamuzi sawa na asilimia 49;

iii. Mahkma ya Kadhi imefunguwa Mashauri 1,670 ambapo Mashauri 1,006 yametolewa uamuzi sawa na asilimia 60.

iv. Mashauri 162 ya Madawa ya kulevya yamefunguliwa ambapo Mashauri 35 yametolewa maamuzi katika kipindi hicho sawa na asilimia 22 ya utekelezaji **(Kiambatanisho nam. 3).**

v. Usajili wa Mawakili kwa njia ya Mtandao umefanyika kwa kutumia mfumo unaoitwa "Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Usimamizi wa Mawakili" (E-Wakili). Mfumo huo pia umesaidia kuwatambua Mawakili bandia pamoja na kuondoa mianya ya kukwepa ulipaji wa kodi kwa Mawakili.

vi. Mahkama kwa kushirikiana na Taasisi ya Taarifa za Kisheria ya Afrika zilitiliana saini makubaliano ya kuendesha mfumo wa kieletroniki wa Zanzibar Lii (ZanLii) ambao utawezesha hukumu za Majaji wanazozitoa kuingizwa moja kwa moja katika mfumo na kuonekana sehemu nyengine. Mfumo huu umeshaanza kutumika na Waheshimiwa Majaji wameshaanza kuziweka katika mfumo huo (uploading) hukumu zao;

vii. Maadhimisho ya Siku ya Sheria yalifanyika tarehe **13/02/2023,** ambapo Mgeni rasmi alikuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa, Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Kauli mbiu ya Maadhimisho hayo ilikuwa ''Haki Mtandao kwa kukuza Uchumi na Ustawi wa Jamii";

viii. Rasimu za kanuni mbili zimetayarishwa kanuni hizo ni: Kanuni ya Malipo ya Mawakili ambayo imeweka viwango sawa vya utozaji wa ada kwa Mawakili wote na Kanuni ya Maadili kwa Maafisa wa Mahkama.

43. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** Mahkama Kuu ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi **9,546,800,000** kwa matumizi ya mishahara na matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi **2023,** Shilingi **6,685,843,320** zimepatikana sawa na asilimia **70.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **5,386,745,250** zilitumika kwa mishahara na **1,299,098,070** zilitumika kwa matumizi mengineyo. Aidha, Mahkama ya Kadhi ilipangiwa kutumiwa ruzuku ya Shilingi **1,266,800,000,** hadi kufikia Machi **2023,** Shilingi **1,050,246,493** zimepatikana sawa na asilimia **83.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **954,446,493** zilitumika kwa mishahara na Shilingi **95,800,000** zilitumika kwa matumizi mengineyo. Aidha, Mahkama ilikadiriwa kukusanya Shilingi **958,552,395** hadi kufikia Machi **2023,** Shilingi **803,591,586** zimekusanywa sawa na asilimia **84, (kiambatanisho nam. 1a and 1c).**

## G03: AFISI YA MWANASHERIA MKUU

Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria

44. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Programu hii unasimamiwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, na katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo;

i. Miswada ya Sheria saba imeandaliwa na Kanuni 23 za Sheria tofauti zimetayarishwa kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa Sheria husika kwa ufanisi;

ii. Mikataba 514 imetolewa ushauri, kati ya hiyo mikataba 335 ya ununuzi wa Bidhaa na Huduma, 95 Ujenzi, 52 Ushauri elekezi na 32 ya kodi. Aidha, Hati za Maelewano (MoU) 107 kuhusu masuala ya elimu, afya, uchumi, usafiri, utalii, makaazi, ardhi, ujenzi, Teknolojia, Kilimo, Utamaduni, Sheria, Mazingira na Fedha zilisainiwa;

iii. Matangazo 70 ya Kisheria yametolewa na tayari yamewasilishwa kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji kwa ajili ya kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali;

iv. Ofisi imeendelea kuiwakilisha Serikali kwenye mashauri 139 ya kesi za madai katika Mahkama mbali mbali na kufuatilia Indhari

za kuishtaki Serikali 32 zilizowasilishwa. Kati ya hizo, kesi 15 zimefunguliwa, kesi 13 zimetolewa hukumu, na kesi 11 Serikali imeshinda na kesi mbili (2) Serikali inaendelea kuyafuatilia maamuzi yaliyotolewa ambapo haikuridhishwa na maamuzi hayo. Kesi 13 zinaendelea kusimamiwa katika Mahkama za Mkoa na mashauri matano (5) Mahkama Kuu.

45. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** Programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi **3,195,300,000** na hadi kufikia Machi **2023,** Shilingi **2,348,292,155** zimepatikana sawa na asilimia **73.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,348,493,355** zimetumika kwa mishahara na Shilingi **999,798,800** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatanisho nam. 1a).**

## G04: AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

### Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai

46. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 kazi zifuatazo zimetekezwa:-

    i. Kesi za jinai 1,385 zimeendeshwa katika Mahakama mbali mbali zilizopo Unguja na Pemba, kati ya hizo kesi 414 za Udhalilishaji, kesi 188 Madawa ya Kulevya, kesi 74

kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, kesi 709 zimehusisha Usalama wa Barabarani, Wizi wa Mazao na Mifugo, wizi baada ya kuaminiwa na Makosa Mengineyo. Aidha, washtakiwa 573 wamekutwa na hatia, 358 wameachiwa huru na kesi 180 zimeondoshwa na Mahakama na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo mashahidi kutofika Mahakamani;

ii. Afisi imefanikiwa kufungua, kusikiliza, kufungwa ushahidi na kutolewa hukumu kwa kesi 174 ndani ya miezi mitatu (Jan-Mach) ikiwa ni mikakati ya Afisi katika kuharakisha usikilizwaji wa kesi na kupunguza mrundikano. Kesi hizo zilihusisha zaidi masuala ya Udhalilishaji na Madawa ya Kulevya;

iii. Majalada 33 ya kesi yamepokewa na majalada 15 yanaendelea na upelelezi, majalada 12 kesi zipo Mahakamani na majalada 6 yamefungwa. Aidha, Waendesha Mashtaka wamekuwa wakifanya vikao na wachunguzi kutoka ZAECA kujadili upelelezi wa majalada ya kesi mbalimbali zilizowasilishwa. Hatua hii, imeimarisha kasi ya uendeshaji wa kesi, utendaji na ushirikiano baina ya taasisi hizi mbili;

iv. Kamati ya Kuzuia Udhalilishaji wa Kijinsia imeanzishwa na inaundwa na wajumbe 25 kutoka taasisi za Serikali na asasi za kiraia na kupatiwa mafunzo. Lengo la Kamati hiyo ni kuanda mipango na mikakati ya kuzuia vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia Zanzibar. Kamati hiyo inatarajiwa kuzinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi;

v. Waendesha Mashtaka wawili wamepatia mafunzo ya muda mrefu ya Shahada ya Pili ya Sheria (LLM). Aidha, watumishi wa Afisi wame patiwa Mafunzo ya muda mfupi kuhusiana na Sheria ya Manunuzi na Uandishi wa Sheria;

vi. Wanafunzi wapya 96 wamedahiliwa katika Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti kwa mwaka wa masomo 2022/2023 kwa ngazi ya cheti na Diploma. Aidha, Utafiti kuhusiana na masuala ya Haki Jinai umefanyika dhidi ya watoto wanaokinzana na Sheria; hasa katika makosa ya udhalilishaji.

47. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023** Programu hii ilipangiwa kutumiajumla ya Shilingi **3,297,900,000,** hadi kufikia Machi **2023** Shilingi **2,316,234,836** zimepatikana sawa na asilimia **66.** Kati ya fedha

hizo, Shilingi **1,865,343,636** zimetumika kwa mishahara na Shilingi **450,891,200** zimetumika kwa matumizi mengineyo. Aidha, ruzuku ya Shilingi **211,500,000** imepangwa kutumika kwa uendeshaji wa Kituo cha Sheria, ambapo hadi kufikia Machi **2023,** ruzuku ya Shilingi **132,000,000** imepatikana sawa na asilimia **62** ya lengo **(kiambatanisho nam. 1a).**

## G05: TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

### Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria

48. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Tume ya Kurekebisha Sheria na katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo:-

    i. Sheria 13 zimefanyiwa mapitio ambazo ni: - Sheria ya Mafuta na Gesi; Sheria ya Ulinzi wa Mimea; Sheria ya Elimu; Sheria ya Wafamasia; Sheria ya Madaktari na Madaktari wa Meno; Sheria ya Utalii; Sheria ya Msaada wa Kisheria; Sheria ya Ndoa na Talaka; Sheria ya Mtoto; Sheria ya Kumlinda Mwari na Mtoto wa Mzazi Mmoja; Sheria ya Utumishi wa Umma; Sheria ya Uanzishwaji wa Chuo cha Mafunzo; na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa. Kwa baadhi ya sheria, mapitio bado yanaendelea;

ii. Ukusanyaji wa maoni juu ya Sheria ya Vyama vya Siasa na Mfumo wa Uchaguzi Tanzania unaendelea;

iii. Kitabu cha Sheria zote zilizopo Zanzibar (Index of Laws) kimechapishwa na mafunzo yametolewa kwa wananchi kuhusu Sheria hizo ili waweze kuzifahamu na kujua malengo na madhumuni ya kutungwa kwake;

iv. Jarida maalum lenye kuelezea athari za udhalilishaji pamoja na vipeperushi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Tume vimeandaliwa na kusambazwa kwa wananchi. Vile vile, kipindi maalum cha ZANZIBAR NA SHERIA kimeandaliwa kwa lengo la kujadili mada mbali mbali zinazohusiana na masuala ya kisheria na kinarushwa moja kwa moja na Shirika la Utangazaji Zanzibar.

**49.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023** Programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi **1,901,790,000.** Hadi kufikia Machi **2023,** Shilingi **933,630,980** zimepatikana sawa na asilimia **69.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **607,987,180** zimetumika kwa mishahara na Shilingi **325,643,800** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatanisho nam. 1a).**

## G12: KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

***Programu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Mirathi, Zakka na Misaada***

50. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana inatekeleza Programu hii na katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 utekelezaji wa kazi ni kama ifuatavyo:-

i. Tirka 1,387 zimefunguliwa kati ya hizo, tirka 743 zenye thamani ya Shilingi **52,433,043,930.3** zimefungwa na warathi kupewa haki zao na majalada 4,540 ya mirathi yanaendelea kushughulikiwa;

ii. Malipo ya wanufaika wa mali za Wakfu na Amana yamesimamiwa ambapo jumla ya Shilingi **58,076,159** zimetumika kulipwa wanufaika pamoja na kufanya matengenezo ya majengo;

iii. Hatua zimeanza kuchukuliwa za kuimarisha mashamba ya Wakfu ambapo jumla ya Shilingi **18,000,000** zimetumika katika kazi hiyo;

iv. Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mali za Wakfu na Amana umeandaliwa na kuanza majaribio ya kuingiza taarifa za mali;

v. Kamisheni imekusanya na kusimamia jumla ya Shilingi **379,000,000** zinazotokana na Zakka, Sadaka na Misaada ya kheri iliyotolewa na waumini;

vi. Wafanyakazi wa Kamisheni wamepatiwa mafunzo juu ya kuimarisha usimamizi wa Zakka na Sadaka. Kupitia mafunzo hayo, Kamisheni imeandaa Mpango wa kuimarisha shughuli za Zakka Zanzibar na tayari imepata ufadhili wa utekelezaji wa Mpango huo;

vii. Kwa upande wa ushughulikiaji wa kesi na mizozo, mashauri 79 yamepatiwa ushauri wa kisheria, mizozo 108 imeshughulikiwa kati ya hiyo 52 imesuluhishwa na 7 inaendelea na hatua za usuluhishi na kesi 45 zimesimamiwa Mahkamani ili kutolewa hukumu;

viii. Kamisheni imeendelea kuratibu safari za Hijja ambapo jumla ya Mahujaji 1,599 wametekeleza Ibada ya Hijja ya mwaka wa 2022. Kamisheni imeshaanza majaribio ya Mfumo wa Mfuko wa Hijja na tayari maandalizi ya kuuzindua yapo katika hatua za mwisho;

ix. Kamati Maalum ya Wataalamu imeundwa kuangalia Muundo na Utendaji wa

Kamisheni na kushauri njia ya kuifanyia mageuzi yatakayoleta tija zaidi katika utekelezaji wa majukumu yake.

51. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** Kamisheni ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi **1,309,750,000.** Hadi Machi 2023, Shilingi **1,169,110,820** zimepatikana, sawa na asilimia **89.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **917,464,910** zimetumika kwa mishahara na Shilingi **251,645,910** matumizi kwa matumizi mengineyo. Aidha, Kamisheni ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi **220,000,00** na imekusanya Shilingi **131,082,610** kutokana na ada ya mirathi sawa na asilimia **60** ya lengo **(Kiambatanisho 1a & 1c)**

**G13: WAKALA WA SERIKALI MTANDAO**

**Programu ya Huduma za Serikali Mtandao**

52. **Mheshimiwa Spika,** Programu wa Huduma za Serikali Mtadao inatekelezwa na Wakala wa Serikali Mtandao na imeendelea kuanda na kuimarisha mifumo ya kielektroniki kwa lengo la kutekeleza dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuleta mageuzi ya teknolojia na kutoa huduma kwa wananchi kwa njia ya kidigitali. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:-

i. Taasisi 146 zimeunganishwa katika mfumo wa barua pepe wa Serikali ili kuwawezesha watendaji wa Taasisi za Umma kutumia email rasmi zinazotambuliwa kwa ajili ya Matumizi ya shughuli za Serikali;

ii. Wakala ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha Mfumo wa Ajira, Mfumo wa Bima ya Afya ya Zanzibar, Mfumo wa Zanzibar ICT Register, Mfumo kiunganishi wa ZanID Middleware na Mfumo wa "One Stop Center" kwa ajili ya Shirika la Bandari pamoja na Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar;

iii. Ukaguzi wa Mifumo 13 umefanyika kwa Taasisi za Serikali kwa lengo la kuhakikisha mifumo hiyo inatumika ikiwa katika hali ya usalama;

iv. Taasisi 62 zimeunganishwa katika mfumo wa ZanMalipo (Generic system) na kukamilisha Taasisi zote zinazotakiwa kuungwa katika Mfumo huo;

v. Mifumo ya fedha (Billing systems) ya Taasisi 21 imeunganishwa na Mfumo wa kielektroniki wa kukusanyia fedha wa ZanMalipo;

vi. Maafisa watatu wamepatiwa mafunzo ya vitendo yanayohusiana na usimamizi na usalama wa mifumo;

vii. Wakala wamekamilisha matayarisho ya Mfumo wa Baketi (MUSE) na Taasisi tano (5) zimechaguliwa kuanza kutumia mfumo huo kama ni sehemu ya majaribio;

viii. Miongozo mitatu (3) ya usimamizi na utekelezaji wa masuala ya Serikali Mtandao Zanzibar (Zanzibar e-Government Guideline) imetayarishwa na kuwasilishwa katika OR-KSUUB kwa ajili ya kuridhiwa na kuwekwa saini.

**53.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023** Wakala wa Serikali Mtandao ilipangiwa jumla ya Shilingi **4,304,000,000.** Hadi kufikia Machi **2023,** Shilingi **1,660,112,625** sawa na asilimia **39.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **871,487,825** zilitumika kwa mshahara na Shilingi **788,624,800** zimetumika kwa matumizi mengineyo. **(Kiambatanisho nam 1a)**

## G14: AFISI YA MUFTI MKUU WA ZANZIBAR

***Programu ya Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Masuala ya Kiislamu***

**54. Mheshimiwa Spika,** Programu inatekelezwa na Afisi ya Mufti Mkuu na katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Afisi ilitekeleza kazi zifuatazo:-

i. Afisi imepokea na kutatua migogoro 871 inayohusu masuala ya ndoa, Talaka, mirathi, migogoro ya kifamilia, misikiti, madrasa mambo mbali mbali ya kidini;

ii. Mafunzo ya maadili ya ndoa yanaendelea kutolewa na wananchi 522 (wanaume 179 na wanawake 343) wamehitimu mafunzo hayo. Aidha, mashekhe 58 wameshiriki katika mkutano uliohusu taratibu za kufungisha ndoa;

iii. Vipindi kuhusiana na masuala mbali mbali ya dini vimetayarishwa na kurushwa kupitia vyombo vya habari kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi;

iv. Mafunzo juu ya Mifumo ya Utoaji Fatwa na Ugawaji wa Zakka yametolewa kwa watumishi wa Ofisi. Mafunzo hayo yalitolewa na wataalamu kutoka Wizara ya Wakfu ya Oman. Ujio wa wataalamu hao ni matunda

yanayotokana na Ziara ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi aliyoifanya Nchini Oman mwezi wa Oktoba 2022;

v. Misikiti 154 imesajiliwa, Madrasa 319 na Misikiti 168 na Madrasa 363 imekaguliwa Unguja na Pemba kwa lengo la kutoa miongozo ya uendeshaji bora kwa taasisi hizo na kuimarisha amani katika sehemu za ibada;

vi. Walimu wa Madrasa 518 (wanaume 293 na wanawake 225) wamepatiwa mafunzo na wamehitimu mafunzo hayo na kupewa vyeti na leseni za ufundishaji. Kati ya hao. Lengo la mafunzo hayo ni kuhakisha uwepo wa walimu wenye maadili na taaluma ya ufundishaji;

vii. Matayarisho ya Mtaala wa kufundishia katika madrasa za Qur-ani yamekamilika na Mtaala upo katika hatua ya kuchapishwa pamoja na Miongozo na Muhutasari ya vyuo vya Qurani.

**55. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi **1,542,200,000.** Hadi kufikia Machi **2023,**

Shilingi **950,090,650** zimepatikana, sawa na asilimia **62.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **698,513,350** zilitumika kwa mishahara na Shilingi **251,577,300** zimetumika kwa matumizi mengineyo. **(Kiambatanisho nam 1a)**

### G15: TUME YA MAADILI YA VIONGOZI

**Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi**

56. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Tume ya Maadili ya Viongozi na katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, kazi zifuatazo zimefanyika:-

    i. Fomu 2,669 za Tamko la Rasilimali na Madeni kutoka kwa viongozi zimepokelewa na kusajiliwa ambapo Viongozi wa Umma 236 wamehakikiwa; (Unguja 188 na Pemba 48). Tume imeendelea kuchukuwa hatua za kisheria kwa viongozi waliochelewa kurejesha fomu hizo. Orodha ya Majina ya Viongozi wote waliowasilisha Fomu kwa mwaka 2022/2023 tayari imechapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali kupitia Tangazo la kisheria nambari 20 la Mwaka 2023;

    ii. Utayarishaji na uimarishaji wa Mfumo wa Kieletroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni unaendelea. Watumishi wote wa Tume wamepatiwa mafunzo ya kutumia

Mfumo huo. Aidha, Tume imeanza kufanyia kazi maoni yaliyotolewa na viongozi kuhusu kuangalia namna gani Fomu ya Tamko la Rasilimali na Madeni inaweza kujazwa na kuwasilishwa Tume ya Maadili kwa njia ya kielektronoki;

iii. Malalamiko 15 ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi yamepokelewa na kufanyiwa kazi. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 12 uchunguzi wake bado unaendelea na malalamiko 2 uchunguzi wake umekamilika na wahusika wanasubiri kuitwa mbele ya Tume kwa ajili ya kusikilizwa utetezi wao, na lalamiko moja tayari limetolewa maamuzi. Malalamiko hayo yanahusiana na matumizi mabaya ya madaraka na uonevu;

iv. Ripoti ya Sita ya Utekelezaji wa Kazi za Tume kwa mwaka 2021/2022 ilitayarishwa na kuwasilishwa kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi tarehe 29 Septemba, 2022 kama sheria zinavyoelekeza. Aidha, Ripoti hiyo iliwasilishwa na kujadiliwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika Mkutano uliofanyika tarehe 15 Disemba, 2022;

v. Mikutano 42 (34 Unguja na 8 Pemba) ya utoaji wa elimu kwa viongozi na umma kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili imefanyika, . Aidha vipindi 4 vya elimu ambavyo vinaelezea Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Mgongano wa Kimaslahi na Maadhimisho ya Siku ya Maadili vimerushwa hewani (ZBC Redio 2 na TV 1);

vi. Tume kwa kushirikiana na taasisi zinazosimamia Utawala Bora nchini imeadhimisha kilele cha Sherehe ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu tarehe 16/12/2022 kwa ufanisi mkubwa. Shughuli mbalimbali zilifanyika kwa lengo la kukuza uelewa na kuhamasisha Viongozi na wananchi kutambua umuhimu wa maadili katika kuimarisha utawala bora nchini.

**57. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** Tume ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi **1,337,800,000.** Hadi kufikia Machi **2023,** Shilingi **880,042,325** zimepatikana sawa na asilimia **66.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **446,294,325** zilitumika kwa mishahara na Shilingi **433,748,000** zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatanisho nam. 1a)**

## E04: AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

### Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa fedha na Rasilimali za Umma

58. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, afisi imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Wizara, Idara na Taasisi za Umma kwa mwaka wa fedha 2021/2022 umefanyika kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji, ukusanyaji wa mapato pamoja matumizi bora ya rasilimali za Umma;

ii. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ipo katika hatua za mwisho kukamilika ili iweze kuwasilishwa katika mamlaka husika kabla ya kuwasilishwa katika mkutano wa Baraza hili Tukufu;

iii. Watendaji 119 wa Afisi ya CAG wamepatiwa mafunzo na Taasisi ya Ukaguzi ya Taifa (National Audit Office) juu ya masuala ya uhasibu na ukaguzi wa viwango vya juu kitaifa na kimataifa pamoja na Mafunzo ya Ukaguzi Jumuishi (Joint Audit). Aidha, watumishi 12 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na kati ya hao, Unguja 7 na Pemba 5.

59. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023** programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya Shilingi **4,801,100,000.** Hadi kufikia Machi **2023,** Shilingi **2,965,988,230** zimepatikana sawa na asilimia **62.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **2,189,865,630** zimetumika kwa ajili ya mishahara na Shilingi **776,122,600** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, Afisi ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi **250,000,000.** Hadi kufikia Machi **2023,** Shilingi **60,744,000** zilizokusanywa sawa na asilimia **24** ikiwa ni ada ya ukaguzi katika taasisi mbali mbali. **(Kiambatanisho nam 1a & 1c)**

### EO5:MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI

***Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi.***

60. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi katika kipindi cha Januari 2022 hadi Machi 2023 ilitekeleza kazi zifuatazo:-

   i. Tuhuma za rushwa na uhujumu uchumi 474 zimepokelewa, na tuhuma 295 kati ya hizo zinaendelea na uchunguzi, 18 zimefungwa, 50 zimefanyiwa udhibiti, 21 zimehamishiwa taasisi nyengine, 90 zimetolewa ushauri, majalada 37 yamewasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa hatua za kisheria, Majalada 19 yalifikishwa Mahakamani, Kesi

5 zilitolewa hukumu Mahakamani, kesi 2 zilikutwa na hatia na Kesi 3 hazina hatia;

ii. Mamlaka imeokoa jumla ya Shilingi 4,027,238,549, kati ya hizo, Shilingi 225,028,000 zimerudi kwa wananchi na Shilingi 3,802,210,549 zimeingizwa katika Mfuko wa Serikali;

iii. Udhibiti umefanyika katika Taasisi mbali mbali za Serikali na imefanikiwa kuokoa Shilingi 558,268,598 za Serikali;

iv. Ufuatiliaji wa miradi yenye thamani ya wastani wa Shilingi 205,308,624,836.01 katika Sekta mbali mbali pamoja na afya, kilimo, elimu, maji n.k., kwa lengo la kuona utekelezaji wake na kutathmini thamani halisi ya fedha katika miradi hiyo.

61. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** Programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi **4,544,600,000.** Hadi kufikia Machi 2023, Shilingi **2,785,839,230** zimepatikana sawa na asilimia **61.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **2,189,865,630** zilitumika kwa mishahara na Shilingi **595,973,600** zilitumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatanisho nam 1a)**

## E07: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

***Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma***

62. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2023, Kamisheni imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Miundo ya Taasisi za Umma 20 imeidhinishwa na Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miundo ya Utumishi umefanyika kwa kuzipitia Wizara zote 18 Unguja na Pemba pamoja;

ii. Nakala 100 za Matoleo ya Miundo ya Utumishi na Miundo ya Taasisi katika Taasisi za Umma imechapishwa;

iii. Ukaguzi wa Kawaida katika Wizara zote za SMZ (18), Taasisi zinazojitegemea (17) Mashirika ya Umma (8) na Kampuni (5) umefanyika kwa lengo la kuangalia Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi na masuala ya Kiutumishi;

iv. Rufaa tatu (3) na Malalamiko matano (5) ya watumishi yamepokelewa na kutolewa uamuzi;

v. Kamisheni pia imefanya Utafiti unaohusu ushiriki wa watu wenye mahitaji maalumu katika Utumishi wa Umma kwa Unguja na Pemba;

vi. Katika kuimarisha mashirikiano na Tume za Utumishi, Kamisheni imefanya mkutano na Makatibu wa Tume hizo kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kutatua changamoto zinazojitokeza katika kutekeleza majukumu ya kazi pamoja na kusisitiza umuhimu wa kusimamia nidhamu kwa watumishi walio chini ya Tume hizo.

vii. Kamisheni imeandaa Rasimu ya Jarida ambalo litasaidia kutoa elimu kuhusu Kamisheni na majukumu yake kwa jumla. Vile vile, Kamisheni imeandaa Ripoti ya Mwaka ya Masuala ya Kifedha na Utekelezaji wa Kazi za Kamisheni ya Utumishi wa Umma inayowasilishwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi. Pia watumishi wanne (4) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na watumishi tisa (9) wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi.

63. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** Kamisheni ilipangiwa jumla ya Shilingi **1,447,300,000.** Hadi kufikia Machi, 2023, Shilingi **855,337,710** zimepatikana sawa na asilimia **59.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **554,910,110** zimetumika kwa mishahara na Shilingi **300,427,600** zimetumika kwa matumizi mengineyo.

## E08: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

### *Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini*

64. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Tume ya Utumishi Serikalini na kipindi cha Julai hadi Machi 2023, kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

    i. Nafasi za ajira 2,709 zimetangazwa kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini na tovuti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Kibali cha ajira kwa watumishi 2,157 kimetolewa kwa Wizara na Taasisi mbali mbali Unguja na Pemba;

    ii. Tume imewathibitisha kazi watumishi 2,182, watumishi 89 wamepandishwa daraja, watumishi 226 wamebadilishwa kada, watumishi wawili (2) wameidhinishiwa nyongeza ya muda wa utumishi, watumishi saba (7) wameidhinishiwa likizo bila ya malipo na watumishi 153 ajira za mkataba. Kadhalika, Tume imeidhinisha kustaafu kwa hiari watumishi wanne (4), Watumishi 714 wamestaafu kazi kwa kufikia umri wa lazima, watumishi 12 wamestaafishwa kwa maradhi. Tume imeridhia kuacha kazi kwa mtumishi mmoja (1) baada ya kwenda kinyume na Sheria na Kanuni na Miongozo ya Utumishi wa Umma na mtumishi mmoja

amerejeshwa kazini **(Kiambatanisho nam 6a & 6b);**

iii. Tume imepokea malalamiko matatu (3) na kuyafanyia kazi. Aidha Tume ya Utumishi imeidhinisha kufukuzwa kazi mtumishi mmoja (1) baada ya kupatikana na kosa la kinidhamu. **(Kiambatanisho 6c)** Vile vile, mafunzo ya Mfumo wa Kielektroniki wa Maombi ya Ajira (ZanAjira) kwa Maafisa utumishi wa Wizara nane (8) na Taasisi tisa (9) za Serikali yametolewa.

**65.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2022/2023,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi **404,702,500.** Hadi kufikia Machi **2023,** Shilingi **379,443,600** zimepatikana, sawa na asilimia **94.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **251,341,200** zilitumika kwa mishahara na Shilingi **128,102,400** zilitumika kwa matumizi mengineyo.

## C. MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**66.** **Mheshimiwa Spika,** naomba sasa kutumia fursa hii kutoa maelezo ya muelekeo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuiwezesha Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria,

Utumishi na Utawala Bora kutekeleza majukumu yake na malengo yalioelezwa katika hotuba hii, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **80,584,431,552.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **51,241,200,000** zitatumika kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na ruzuku (**Shilingi 33,314,387,980** mishahara, Shilingi **17,926,812,020** matumizi mengineyo na Ruzuku), na Shilingi **29,343,231,552** zitatumika kwa Miradi ya Maendeleo (Shilingi **1,000,000,000** ni utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma; Shilingi **969,631,552** ikiwa ni mchango kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa Mradi wa Uwezeshaji na Upatikanaji wa Haki awamu ya pili; Shilingi **373,600,000** ni mchango wa Washirika wa Maendeleo kwa Mradi wa Upatikanaji wa Haki kwa Wanawake katika Kesi za Udhalilishaji; Shilingi **25,000,000,000** kwa Mradi wa ujenzi wa Mahkama za Mikoa na Wilaya na Shilingi **2,000,000,000** kwa Mradi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Mahkama). (**Kiambatanisho namb 2).**

68. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imepangiwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali Shilingi **4,535,900,000** kupitia vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. **(Kiambatanisho nam 1c).**

69. **Mheshimiwa Spika,** Kabla ya kuendelea mbele naomba nielekeze kwamba tunatayarisha Bajeti kwa mwaka huu 2023/2024, ikiwa tayari

tumepokea matokeo ya Sensa ya Watu na Makaazi ya Mwaka 2022 kwa hivyo, naomba niwahahakishie Wananchi kwamba, Afisi ya Rais- Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora itazingatia ipasavyo matumizi ya takwimu za Sensa za Watu na Makaazi katika kutoa huduma kwa Wananchi katika ngazi zote za Taifa, Mikoa, Wilaya na Shehia. Vile vile, katika utayarishaji mpango kazi kwa kila Idara na Taasisi tutazingatia masuala ya kijinsia kwa lengo la kuimarisha usawa na utoaji wa haki kwa wananchi. Tutatekeleza mambo haya kama yanavyosisitizwa na Serikali na kwa kuzingatia ushauri wa washirika wetu wa maendeleo. Kwa mara nyengine, natoa pongezi kwa Taasisi zote na wahusika walioshiriki katika kufanikisha zoezi la Sensa ya Watu na Makaazi ya Mwaka 2022.

## D.VIPAUMBELE VYA AFISI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

70. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

    i. Kutekeleza Mpango wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria Awamu ya Pili;

    ii. Kuendelea na Utekelezaji wa Mpango wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma Awamu ya Pili;

iii. Kushughulikia Maslahi ya watumishi wa Umma, Miongozo na Matoleo ya Kiutumishi pamoja na Miundo ya Kiutumishi ya Taasisi;

iv. Kuendeleza matumizi wa Mifumo ya Kieletroniki katika utumishi wa Umma;

v. Kutayarisha na kutoa miongozo ya Utoaji wa Msaada wa Kisheria na kuandaa Mpango kazi wa Kitaifa (NPA);

vi. Kuongeza wigo wa upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi waliowengi na walio katika mazingira duni;

vii. Kuendelea kuimarisha utendaji katika taasisi za Sheria na kufanya marekebisho ya sheria mbali mbali;

viii. Kuunganisha Mfumo wa Malipo na Mfumo wa Utumishi awamu ya pili katika Taasisi na Mashirika;

ix. Kuendelea kuimaraisha umoja na mshikamano pamoja kudumisha Amani na Utulivu kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali.

x. Kusimamia Maadili katika utumishi wa umma na misingi ya utawala bora

xi. Kuongeza kasi katika mapambano dhidi ya

vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma;

xii. Kuongeza kasi katika Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma;

***Malengo Makuu ya Afisi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024***

**71. Mheshimiwa Spika,** ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vya Afisi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Afisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Kuimarisha upatikanaji wa haki na utawala wa sheria;

ii. Kusikiliza kesi na kutoa maamuzi ya haraka na kwa wakati;

iii. Kuhakikisha Upatikanaji wa Msaada wa Kisheria katika maeneo yote ya kijamii;

iv. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Rasilimaliwatu wa mwaka 2023/2024;

v. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa mafunzo ya watumishi wa umma kwa ajili ya upatikanaji wa Rasilimali Watu wenye sifa;

vi. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika shughuli na utoaji wa huduma za Serikali na kukuza uchumi;

vii. Kuimarisha misingi ya utawala bora na maadili katika utendaji wa shughuli za Serikali; na

viii. Kuogeza kasi katika usimamizi na udhibiti na rasilimali za mali za Serikali.

**72.** **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya sasa naomba kuwasilisha maelezo ya programu za Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama ifuatavyo:-

**73.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inatekeleza jumla ya mafungu ya bajeti 13 kupitia Programu kuu 16 kama ifuatavyo: i) Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria; ii) Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora; iii) Programu ya Uratibu na Uendeshaji wa ARKSUUB; na iv) Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma ziliomo katika fungu **G01** v) Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki **G02;** vi) Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria **G03;** vii) Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai **G04,** viii) Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria **G05;** ix)

Programamu ya Haki na Uwezeshaji Kisheria **G12;** x) Programu ya Huduma za Serikali Mtandao **G13;** xi) Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini **G14;** xii) Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi wa Umma **G15;** xiii) Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma **E04;** xiv) Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi **E05;** xv) Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma **E07;** xvi) Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini **E08.**

74. **Mheshimiwa Spika,** kati ya programu hizi, programu kuu nne (4) za fungu **G01** zinasimamiwa na kutekelezwa kupitia Idara zilizo chini ya Katibu Mkuu na Programu Kuu **12** zinatekelezwa na Taasisi zinazojitegemea.

## G01:AFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

**Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria.**

75. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuendesha Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia kwa lengo la kuongeza wigo wa upatikanaji wa msaada wa kisheria;

ii. Itafanya mapitio ya mfumo wa usajili wa watoaji msaada wa kisheria pamoja;

iii. Itafanya mapitio ya Sera ya Msaada wa Kisheria ya mwaka 2017 na Sheria ya Msaada wa Kisheria Nam.13 ya mwaka 2018;

iv. Itaanzisha mfumo wa upatikanaji wa msaada wa kisheria kiganjani (legal aid app);

v. Idara itaandaa mikutano mbali mbali ya wahusika wa masuala ya udhalilishaji na utoaji wa mafunzo ya ushauri nasihi wa waathirika wa vitendo vya udhalilishaji;

vi. Itachapisha Jarida la Msaada wa Kisheria na Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Msaada wa Kisheria (NPA). Aidha, itashiriki vikao mbali mbali vya haki za binadamu vya kitaifa na kikanda.;

vii. Mafunzo ya kujengea uwezo wa watendaji yafatolewa sambamba na ziara za kujenga mahusiano na mashirikano kwa taasisi zenye malengo sawa na Idara.

**76. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2023/2024,** idara imetengewa Shilingi **222,333,200** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatanisho nam 2)**

***Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora.***

77. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024, programu ya usimamizi wa Utawala Bora inayosimamiwa na Idara ya Utawala Bora imepanga kutekeleza yafuatayo;

    i. Kuijengea uwezo jamii kuhusu masuala mbalimbali ya Utawala Bora;

    ii. Kuanzisha Sheria ya Usimamizi wa Utawala Bora, Kufanya tathmini mbali mbali za Utawala Bora.

78. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Idara kutekeleza programu hii kwa mwaka wa fedha **2023/2024,** Shilingi **316,566,320** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatanisho nam 2)**

***Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ARKSUUB***

79. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, programu ya Uendeshaji na Utumishi imepanga kutekeleza yafuatayo:-

    i. Kupima utendaji kazi na kuwapatiwa stahiki sahihi watumishi kwa lengo la kukuza uwajibikaji, kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Ununuzi, kusimamia Mpango wa Ukaguzi wa Hesabu wa Ndani sambamba

na kusimamia Mfumo wa Mahudhurio ya Kielektroniki ulioazishwa ili kuongeza uwajibikaji wa watumishi;

ii. Idara itafanya mapitio wa Mkataba wa Utoaji wa Huduma wa Ofisi na kujenga uwezo kwa Taasisi na Wizara juu ya utekelezaji na Mkataba huo;

iii. Kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi wa Wizara na kuimarisha mazingira bora ya utendaji wa kazi kwa kuwapatia watumishi vifaa na nyezo za kufanyia kazi.

80. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Idara kutekeleza programu hii ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2023/2024**, imepangiwa kutumia Shilingi **2,745,301,480** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatanisho nam 2)**

81. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti imepanga kufanya yafuatayo katika mwaka wa fedha 2023/2024:-

i. Kuratibu mapitio na matayarisho ya Sera, Sheria, na utekeleezaji wa mipango ya bajeti sambamba na kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa kazi za Wizara;

ii. Kuratibu tafiti za sekta ya Sheria, utumishi na Utawala Bora na kuandaa nyaraka za kisera na kisheria zitakazowasilishwa Serikalini;

iii. Idara itaratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Sheria na Programu ya Mpango wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma wa Awamu ya Pili kupitia utekelezaji wa Programu ya Upatikanaji wa Haki za Wanawake katika eneo la kesi za Udhalilishaji (Gender Responsive Access to Justice for Women Respond against GB cases) na Programu ya Uwezeshaji wa Kisheria na Upatikanaji wa Haki Awamu ya pili (Legal Empowerment & Acees to Justice). Programu hizi zitatekelezwa kupitia ufadhili wa Mashirika ya Maendeleo ambao ni UNDP na UN-Women.

82. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2023/2024,** Idara imepangiwa kutumia Shilingi **339,462,960** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatanisho nam 2).**

83. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Afisi Kuu Pemba itaendelea kuratibu na kusimamia shughuli zote za utawala na utumishi, mipango na bajeti zinazotekelezwa na Afisi kwa upande wa Pemba.

84. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2023/2024,** Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi **510,024,020** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatanisho nam 2).**

***Programu ya Uendelezaji wa Watumishi wa Umma.***

85. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Watumishi wa Umma inahusisha Programu ya Mipango na Maendeleo ya Watumishi na Programu ya Miundo na Mifumo ya Taasisi zinazotekelezwa kupitia Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu na Maendeleo na Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi.

86. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Programu ya Mipango na Maendeleo ya Watumishi imepanga kufanya yafuatayo:-

i. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma;

ii. Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Taasisi za Umma na upatikanaji wa mafunzo yanayotolewa na Washirika wa Maendeleo;

iii. Kuzipatia mafunzo Taasisi za Umma juu ya matumizi Mfumo wa Rasilimali Watu na Malipo ya Mishahara, na kufuatilia utendajikazi wa Mfumo;

iv. Kufanya ukaguzi wa matumizi ya rasilimaliwatu katika Taasisi za Umma (Staff Audit) na kuwapanga watumishi kwa mujibu wa mahitaji na taaluma zao;

v. Kukamilisha Mfumo wa Maombi ya Ajira (ZanAjira) na kutoa vibali vya ajira;

vi. Kusimamia matayarisho ya Kanuni za Kimaadili kwa Sekta za Taaluma.

**87. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2023/2024** Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi **635,667,400** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatanisho nam 2).**

**88. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Miundo na Mifumo ya Taasisi ambayo inatekelezwa na Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kufanya mapitio ya Miundo ya Taasisi za Serikali kwa kuzingatia Hati Idhini ya Serikali zilizotolewa;

ii. Kufanya mapitio ya Fomu za Upimaji wa wafanyakazi kwa kuanzisha Mfumo wa Kieletroniki wa Upimaji wa wafanyakazi (Performance Apprisal System) na kuifanyia majaribio;

iii. Kuandaa Mkataba wa Upimaji Utendaji kazi kwa Viongozi (Performance Contracts) na kuifanyia majaribio;

iv. Kufanya mapitio ya Mkataba wa utoaji wa Huduma kwa Wateja na kusimamia utekelezaji wake.

89. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi 713,044,620 kwa matumizi ya kazi za kawaida. (Kiambatanisho nam 2)

**TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU- G01**

***Chuo Cha Utawala wa Umma***

90. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Chuo Cha Utawala wa Umma kimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendesha mafunzo ya kujenga uwezo wa watumishi wa Umma pamoja na kutoa mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia maadili na misingi ya uwajibikaji;

ii. Kufanya Tafiti katika Utumishi wa Umma ili kubaini mapungufu yaliyopo katika sekta ya umma na kutoa huduma ya ushauri elekezi kwa taasisi zitakazo hitaji huduma hizo;

iii. Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi wa Umma na wananchi wengine katika ngazi ya Shahada, Stashahada na Astashahada.

91. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2023/2024,** Chuo kimepangiwa ruzuku ya Shilingi **2,386,900,000** kwa ajili ya mishahara. Aidha, Chuo kimepanga kukusanya Shilingi **2,035,900,000** kutokana na malipo ya ada za wanafunzi **(Kiambatanisho nam 2)**

**Skuli ya Sheria Zanzibar**

92. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Skuli ya Sheria Zanzibar kupitia Programu ya Mafunzo ya Sheria kimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

    i. Kutoa mafunzo ya vitendo kwa wahitimu wa fani ya sheria kutoka Vyuo Vikuu katika ngazi ya Shahada ya kwanza;

    ii. Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wanasheria waliomo ndani na nje ya Serikali, waheshimiwa Majaji, Mahakimu, Makadhi, Mawakili, Wasaidizi wa Sheria pamoja na watoa Msaada wa Kisheria.

93. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Skuli ya Sheria kutekeleza programu hii kwa mwaka wa fedha **2023/2024,** imepangiwa kutumia Shilingi **370,600,000** kwa ajili ya ruzuku ya matumizi mengineyo. Aidha, Skuli ya Sheria imepanga kukusanya Shilingi **259,000,000** kupitia malipo ya ada za wanafunzi na uendeshaji wa mafunzo mafupi. **(Kiambatanisho 2)**

## G02: MAHKAMA KUU

### Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki

**94. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 Mahkama imepanga kutekeleza kazi zifuatazo;

i. Kuongeza kasi ya usikilizaji wa kesi na utoaji maamuzi kwa wakati;

ii. Kuendeleza matayarisho ya mfumo wa kieletroniki wa mahakama (e-Mahakama) na kujenga uwezo wa wadau wote juu ya matumizi ya mfumo huo;

iii. Kujenga na kuyafanyia matengenezo majengo ya Mahkama Unguja na Pemba.

**95. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Mahakama kutekeleza Programu hii kwa ufanisi, kwa mwaka wa fedha **2023/2024**, imepangiwa kutumia Shilingi **12,911,500,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya hizo, Mahkama ya Kadhi imepangiwa kutumia Shilingi **1,681,000,000.** Aidha, Mahkama imepangiwa kukusanya mapato ya Shilingi **1,576,000,000.** Miradi ya Maendeleo Mahkama imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi **25,000,000,000** kwa Mradi wa ujenzi wa Mahkama za Mkoa na Wilaya na Shilingi **2,000,000,000** kwa Mradi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Mahkama. **(Kiambatanisho nam 2&3)**.

## G03: AFISI YA MWANASHERIA MKUU

### *Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa huduma za Sheria*

96. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia programu hii itatekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuimarisha mfumo wa Sheria kwa kutayarisha, kuhifadhi na kusimamia masuala yanayohusu uandishi wa Sheria, Kanuni na Matangazo ya Kisheria;

ii. Kuendelea kusimamia na kutekeleza Mikataba ya Serikali kikanda na kimataifa pamoja na kutoa ushauri wa kisheria katika Hati za Maelewano (MoU);

iii. Kuendelea kuiwakilisha Serikali Mahkamani dhidi ya Kesi zote za Madai, kufuatilia indhari za kuishtaki Serikali pamoja na kufanya Uchambuzi na Ushauri katika masuala mbali mbali ya Kesi za Madai;

iv. Kufanya Mapitio ya Sheria za Zanzibar pamoja na kuzichapisha. Afisi pia itaendelea kuwajengea Uwezo wafanyakazi kwenye Uandishi wa Sheria, Usimamizi wa Kesi na masuala ya Mikataba.

97. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2023/2024,** Programu hii imepangiwa kutumia Shilingi **3,368,000,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida **(Kiambatanisho nam 2)**

## G04: AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

***Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa kesi za jinai***

98. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika ushughulikiaji wa majalada, uendeshaji wa mashtaka na usalama wa Ofisi kwa lengo la kuongeza ufanisi;

ii. Kuimarisha miundombinu na huduma za Ofisi katika ngazi za mikoa na wilaya ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kimashtaka;

iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa kada mbali mbali kwa kuwapatia Mafunzo mahsusi (Specialized Training) na nyenzo za kutendea kazi ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji yaliopo;

iv. Kushirikiana na Taasisi mbali mbali katika kutoa elimu pamoja na kuziba mianya inayopelekea kuendelea kutokea kwa makosa ya udhalilishaji wa kijinsia;

v. Kufanya utafiti katika masuala ya kimashtaka na haki jinai kwa ujumla;

vi. Kadhalika, Afisi itaendelea kuimarisha ushirikiano na Taasisi za uchunguzi wa makosa jinai ili kuimarisha utaalamu katika eneo hilo.Vile vile, itakiimarisha kitengo cha Haki za Binaadamu, na itasimamia Kamati ya Kuzuia Udhalilishaji wa Kijinsia.

99. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kutekeleza majukumu yake ipasavyo, kwa mwaka wa fedha **2023/2024,** Shilingi **3,780,400,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Aidha ruzuku ya Shilingi **158,700,000** imepangwa kutumika kwa ajili ya Chuo cha Utafiti wa Sheria. **(Kiambatanisho nam 2).**

**G05: TUME YA KUREKEBISHA SHERIA**

**Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria**

100. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Kurekebisha Sheria kupitia programu hii imepanga kutekeleza yafuatayo;-

i. Kutoa elimu ya Sheria kwa wananchi na wahusika wengine kwa kutumia njia bora na za kisasa;

ii. Itaendelea kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuimarisha stahiki zao;

iii. Kuimarisha na kuongeza nguvu ya utendaji katika Afisi ya Tume Pemba;

iv. Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Tume kwa mujibu wa Muongozo uliotolewa na Tume ya Mipango ya Afisi ya Rais Fedha na Mipango;

v. Kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni zinazotumika katika Taasisi za Serikali.

**101. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Tume kutekeleza programu hii ipasavyo, kwa mwaka wa fedha **2023/2024** imepangiwa kutumia Shilingi **1,866,700,000** kwa matumizi ya kawaida **(Kiambatanisho nam 2)**

### G12: KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

***Programu ya Haki na Uwezeshaji Kishariah***

**102. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2023/2024 Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuimarisha na kuendeleza mali za Wakfu na Amana ili zitoe manufaa makubwa zaidi;

ii. Kuimarisha upatikanaji wa Haki kupitia mirathi na utatuzi wa migogoro sambamba na kuiwezesha Baytul-mal kupunguza umasikini;

iii. Kuimarisha mikakati ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia Zakka, Sadaka na misaada ya kheri inayotolewa na jumiya na taasisi mbali mbali za ndani na nje ya nchi;

iv. Kuimarisha huduma za Hijja, Umrah na Ziara za utalii wa Kiislamu;

v. Kuendelea kuimarisha matumizi ya Mifumo ya Kieletroniki na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kutoa huduma mbali mbali za Mirathi, Hijja. Zaka nk.

**103.** **Mheshimiwa Spika,** ili Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, kwa kipindi cha mwaka wa Fedha **2023/2024** imepangiwa kutumia Shilingi **1,930,100,000** kwa mishahara na kazi za kawaida. Kati ya hizo, Shilingi **1,347,600,000** zitatumika kwa mishahara na Shilingi **582,500,000** kwa matumizi mengineyo. Aidha, jumla ya Shilingi **220,000,000** za ushuru wa Mali maiti zinatarajiwa kukusanywa ili kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali.

## G13: WAKALA WA SERIKALI MTANDAO

### Programu ya Huduma za Serikali Mtandao

104. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wakala wa Serikali Mtandao imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kufanya mapitio ya Sera ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2012;

ii. Kutayarisha Mkakati wa Kidigtali wa Zanzibar pamoja na Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Wakala wa Serikali Mtandao;

iii. Kujenga uwezo wafanyakazi wa Wakala wa Serikali Mtandao katika utumiaji wa mifumo ya TEHAMA;

iv. Itaimarisha Miundombinu ya Pamoja (shared infrastructure) ya Serikali Mtandao;

v. Kuimarisha usalama wa mifumo pamoja na kuandaa miongozo mbali mbali;

vi. Itaongeza nguvu ya kushirikiana na taaisisi zinahusika na ukusanyaji wa mapato na zilizo mstari wa mbele katika vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa uchumi.

105. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2023/2024,** Wakala imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi **3,208,600,000,** kati ya fedha hizo, Shilingi **1,249,700,000** ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi **1,958,900,000** ni kwa Matumizi ya kawaida. **(Kiambatanisho nam 2)**

**G14: AFISI YA MUFTI MKUU WA ZANZIBAR**

**Programu ya Usimamizi wa Masula ya Dini**

106. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar kupitia Programu ya Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Masula ya Kiislamu imepanga kufanya yafuatavyo katika mwaka ujao wa fedha 2023/2024;-

i. Kutoa fatwa na kuhakikisha uwepo wa usimamizi mzuri wa masuala ya Kiislamu;

ii. Kuendelea kutoa miongozo juu ya masuala mbali mbali ya Kiislamu, ikiwa ni pamoja na kusimamia Misikiti, Madrasa na Walimu wa Madrasa kwa mujibu wa Sheria ilioanzisha taasisi hiyo;

iii. Kuratibu na kusimamia uandaaji wa mihadhara, warsha, semina na mikutano ya Kiislamu, sherehe na maadhimisho ya Kiislamu na kutangaza kuandama kwa mwezi kwa mujibu wa Sheria;

iv. Kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya masuala mbalimbali ya Kiislamu kupitia vyombo vya habari.

v. Kuratibu kazi za kitafiti za Kiislamu zinazoandaliwa na Taasisi za Serikali na binafsi.

107. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Afisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar kutekeleza programu yake ipasavyo, kwa mwaka wa fedha **2023/2024**, imepangiwa kutumia **Shilingi 1,822,100,000** kwa kazi za kawaida **(Kiambatanisho nam 2)**

## G15: TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

***Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi***

108. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Itaendelea kupokea, kuhifadhi na kusajili taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma pamoja na kupokea malalamiko na kufanya uchunguzi wa uvunjwaji wa Sheria ya Maadili;

ii. Itaendelea kuhakiki taarifa za mali na madeni za viongozi wa umma na kuelimisha viongozi wa umma na wananchi kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili;

iii. Vile vile, itaadhimisha Siku ya Maadili Duniani na itawapatia mafunzo mbalimbali watumishi wa ngazi mbali mbali;

iv. Itaendela kupokea na kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu malalamiko na madai ya uvunjaji wa maadili ya viongozi wa umma;

v. Kukamilisha Mfumo wa Kieletroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni

**109. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha **2023/2024,** Tume ya Maadili imepangiwa kutumia Shilingi **1,301,100,000** kwa matumizi ya kawaida.

## E04: AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

***Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma***

**110. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Afisi imepanga kufanya yafuatayo:-

i. Afisi itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kikatiba ya kukagua mahesabu ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwa ni pamoja na Wizara, Mashirika na Taasisi mbali mbali pamoja na Miradi ya Maendeleo;

ii. Kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kitaaluma katika fani mbali mbali.

**111. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Afisi kutekeleza programu yake ipasavyo, kwa kipindi cha mwaka wa fedha **2023/2024,** Ofisi imepangiwa kutumia jumla ya Shilingi **6,292,400,000** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. Aidha, Afisi imepangiwa kukusanya makadirio ya shilingi **325,000,000. (Kiambatanisho nam 2&3)**

**E05: MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI**

***Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi***

**112. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka itaelekeza nguvu zake katika Udhibiti wa vitendo vya rushwa katika ununuzi wa umma, ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali pamoja na katika maeneo ya huduma za kijamii. Itaendelea kufuatilia utekekelezaji wa miradi ya maendeleo, kuendelea kufanya uchunguzi

wa vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Pia, itaendelea kutoa elimu juu ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi ili kuhakikisha fedha za Serikali zinatumika kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa.

113. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi kutekeleza programu yake ipasavyo, kwa mwaka wa fedha **2023/2024,** jumla ya Shilingi **4,294,600,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatanisho nam 2)**

## E07: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

### Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma

114. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Kamisheni imepanga kuendelea na kufanya Uchambuzi wa Miundo ya Taasisi na Miundo ya Utumishi 24 itakayowasilishwa Kamisheni. Aidha, itaendelea kuandaa Muongozo unaohusiana na ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu katika utumishi wa Umma. Kamisheni pia itafanya zoezi la kupita katika Taasisi za Umma kwa ajili ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Miundo ya Taasisi iliyoidhinishwa na Kamisheni.

**115. Mheshimiwa Spika,** Katika hatua nyengine ya usimamizi wa Utumishi wa Umma Kamisheni itafanya Ukaguzi wa kawaida katika Taasisi za Umma 31, Ukaguzi maalum katika Taasisi 4 na ukaguzi wa kushtukiza katika baadhi ya taasisi Unguja na Pemba. Kamisheni pia itapokea na kushughulikia rufaa na malalamiko kutoka kwa watumishi na mamlaka za nidhamu. Kadhalika itaanda Ripoti ya Hali ya Utumishi wa Umma na itafanya Tafiti inayohusu ufanisi wa mashine ya mahudhurio (Biometric) katika usimamazi wa mahuduhurio ya watumishi. Vile vile. itawapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi Watumishi wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma pamoja na Kufanya mikutano na Mamlaka za ajira kuhusu masuala mbali mbali ya kiutumishi. Kadhalika, itaendelea Kuielimisha jamii kuhusu Kamisheni ya Utumishi wa Umma na Majukumu yake kupitia vipindi vya Televisheni na Redio.

**116. Mheshimiwa Spika,** Ili kuiwezesha Kamisheni ya Utumishi wa Umma kutekeleza programu yake ipassvyo, kwa Mwaka wa Fedha **2023/2024** jumla ya Shilingi **1,249,800,000** zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatanisho nam 2)**

## E08: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

### Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa watumishi Serikalini

**117. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Tume itaendelea na kusimamia shughuli za uajiri kwa kuzingatia sifa na vigezo vinavyostahiki. Aidha, inaendelea kusimamia haki na nidhamu za watumishi wa Serikali ikiwa ni pamoja na kupokea na kusikiliza malalamiko ya watumishi wasioridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka za Nidhamu zilizo chini ya usimamizi wa Tume. Tume itaendelea Kuratibu uidhinishwaji wa ajira za mkataba, kuthibitisha kazi watumishi, kubadilisha kada, kupandisha daraja, kutoa nyongeza za muda wa utumishi, likizo bila ya malipo na kustaafisha kisheria watumishi wa Serikali.

Sambamba na hilo, kuimarisha huduma za kiutawala na za kiuendeshaji na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi wafanyakazi wa Tume ya Utumishi Serikalini ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

**118. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Tume ya Utumishi Serikalini kutekeleza programu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha **2023/2024,** jumla ya Shilingi **867,700,000** zimepangwa

kutumika kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida. **(angalia kiambatanisho nam 2).**

## E. SHUKRANI

**119. Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, natoa shukurani zangu za dhati kabisa wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 katika utekelezaji wa majukumu yetu. Shukrani za pekee ziwaendee Washirika wa Maendeleo walioendelea kushirikina nasi katika kutekeleza programu na mipango yetu ya uimarishaji wa sekta ya Sheria, Utumishi na Utawala Bora na kuleta maendeleo. Naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwataja wachache ambao ni: Jamhuri ya Watu wa China, Korea ya Kusini, India, Saudia Arabia, Oman, Ireland, Malaysia, Switzerland na Uingereza. Mashirika ya Kimataifa ni pamoja na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (UNDP), Jumuiya ya Kimataifa ya Wanawake (UN Women), Kituo cha Watoa Huduma za Kisheria (Legal Service Facility), Benki ya Dunia (World Bank), Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IDB), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuzuia Uhalifu na Madawa ya Kulevya (UNODC) na Jumuiya ya Kiafrika ya Uongozi na Utawala wa Umma (AAPAM).

120. **Mheshimiwa Spika,** nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru viongozi wenzangu na nikianza Ndugu. Mansura Mosi Kassim, Katibu Mkuu, Ndugu. Omar Haji Gora, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wakuu wote wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Mtendaji Mkuu wa Mahkama na Warajis, Waheshimiwa Majaji na Mahakimu wote, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na Naibu wake, Mkurugenzi wa Mashataka na Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Naibu wake, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Mufti Mkuu na Kadhi Mkuu kwa kuendelea kusimamia utoaji wa haki kwa haraka na ufanisi wa hali ya juu.

121. **Mheshimiwa Spika,** nawashukuru, Wenyeviti wa Tume na Kamisheni, Makamishna na Wajumbe wote waliomo katika taasisi hizi, Wakuu wa Vitengo pamoja na wafanyakazi wenzangu wote wa Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora na taasisi zake kwa kuendelea kujituma kwa juhudi na maarifa katika kutekeleza malengo na majukumu ya Afisi yetu. Niwaombe tuendelee kushirikiana katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku na kuhakikisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi na utoaji wa haki kwa wakati.

**122. Mheshimiwa Spika,** natoa shukrani za pekee kwa Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi mbali mbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kushirikiana kwa karibu katika kutekeleza majukumu yetu. Juhudi zetu za pamoja ni muhimu katika kudumisha Muungano wetu.

**123. Mheshimiwa Spika,** kipekee tuwashukuru wahusika wote wa Sekta ya Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao wametupatia ushirikiano wa kutosha katika kuendeleza Sekta hii. Shukrani zangu za pekee nazitoa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wafanyakazi wote kwa kuchapa vizuri hotuba hii.

## F. HITIMISHO

**124. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki cha utekelezaji Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imetekeleza majukumu yake ya msingi kwa kuzingatia Bajeti na Mpango Kazi wa Afisi wa Mwaka 2022/2023, Sera, Sheria na Miongozo mbali mbali ya Serikali. Kwa pamoja, tumefanya jitihada kubwa katika kuhakikisha upatikanaji wa haki, maslahi ya watumishi, usimamizi wa utawala bora, maadili ya viongozi wa umma, udhibiti wa vitendo vya rushwa, utayarishaji wa mifumo na utoaji wa huduma kwa wananchi.

125. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka **2023/2024,** Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora itaendelea kusimamia na kutekeleza majukumu yake yote hayo muhimu katika uendeshaji wa nchi yetu, kuimarisha utawala bora na upatikanaji wa haki kwa wakati ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Sheria, Utumishi na Utawala Bora inaendelea kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa demokrasia na uchumi wa nchi yetu.

126. **Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuiwezesha Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kutekeleza majukumu yake na malengo yalioelezwa katika hotuba hii, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **80,584,431,552.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **51,241,200,000** zitatumika kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na ruzuku (Shilingi **33,314,387,980** mishahara, Shilingi **17,926,812,020** matumizi mengineyo na Ruzuku), na Shilingi **29,343,231,552** zitatumika kwa Miradi ya Maendeleo (Shilingi **1,000,000,000** ni utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma; Shilingi **969,631,552** ikiwa ni mchango kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa Mradi wa Uwezeshaji na Upatikanaji wa Haki awamu ya pili; Shilingi **373,600,000** ni mchango wa Washirika wa Maendeleo kwa Mradi wa

Upatikanaji wa Haki kwa Wanawake katika Kesi za Udhalilishaji; Shilingi **25,000,000,000** kwa Mradi wa ujenzi wa Mahkama za Mikoa na Wilaya na Shilingi **2,000,000,000** kwa Mradi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Mahkama).

**127. Mheshimiwa Spika,** Wizara imepangiwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali Shilingi **4,535,900,000** kupitia vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

**128. Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwasilisha.

**MWAL. HAROUN ALI SULEIMAN**
***Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.***
**ZANZIBAR.**

| **MAPITIO** | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kiambatanisho nambari 1a: Muhtasari wa Upatikanaji wa fedha 2022/2023 (katika,000)** | | | | | | | | | |
| **MAKADIRIO KWA MWAKA 2022/2023** | | | | | **FEDHA ZILIZOPATIKANA KWA MWAKA 2022/2023** | | | | |
| **PROGRAMU KUU/ PROGRAMU NDOGO** | **MISHAHARA** | **MATUMIZI MENGINEYO** | **JUMLA YA FEDHA ZILIZOKADIRIWA** | **MISHAHARA** | **MATUMIZI MENGINEYO** | **JUMLA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA** | **% MISHAHARA** | **% OC** | **% SA +OC** |
| **Programu ya Masula ya Kisheria** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Masuala ya Kisheria | 74,200,000 | 209,040,000 | **283,240,000** | 78,515,860 | 74,702,654 | **153,218,514** | 105.82 | 35.74 | 54.09 |
| **Jumla ya Programu** | | | **283,240,000** | | | **153,218,514** | | | **54.09** |
| | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utawala Bora | 141,500,000 | 164,853,000 | **306,353,000** | 150,061,770 | 50,202,621 | **200,264,391** | 106 | 30 | 65 |
| **Jumla ya Programu** | | | **306,353,000** | | | **200,264,391** | | | **65** |
| | | | | | | | | | |
| **Programu ya Uendshaji na Uratibu wa ORKSUUB** | | | | | | | | | |
| Uendeshaji na Utawala | 978,699,000 | 1,606,675,000 | **2,585,374,000** | 1,207,628,180 | 1,045,378,445 | **2,253,006,625** | 123 | 65 | 87 |
| Mipango,Sera na Utafiti | 160,000,000 | 203,010,000 | **363,010,000** | 126,511,150 | 62,578,155 | **189,089,305** | 79 | 31 | 52 |
| Uratibu wa ORKSUUB- Pemba | 372,473,000 | 200,100,000 | **572,573,000** | 225,628,870 | 51,527,810 | **277,156,680** | 61 | 26 | 48 |
| **Jumla ya Programu** | | | **3,520,957,000** | | | **2,719,252,610** | | | **77** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Uendelezaji wa Utumishi wa Umma** | | | | | | | | | |
| Mipango na Maendeleo ya Watumishi | 170,000,000 | 302,210,000 | **472,210,000** | 252,031,587 | 122,000,892 | **374,032,479** | 148 | 40 | 79 |
| Miundo na Mifumo ya Taasisi | 310,000,000 | 233,000,000 | **543,000,000** | 380,388,733 | 102,186,333 | **482,575,066** | 123 | 44 | 89 |
| **Jumla ya Programu** | | | **1,015,210,000** | | | **856,607,545** | | | **84** |
| Jumla ya Programu -G01 | | | **5,125,760,000** | | | **3,929,343,060** | | | **77** |
| **Ruzuku G01** | | | | | | | | | |
| Chuo Cha Utawala wa Umma | 1,380,700,000 | 53,000,000 | **1,433,700,000** | 1,800,649,620 | 53,000,000 | **1,853,649,620** | 130 | 100 | 129 |
| Skuli ya Sheria | | 529,500,000 | | | 250,251,800 | 250,251,800 | | 47 | |
| **Jumla ya Ruzuku -G01** | | | **1,433,700,000** | | | **2,103,901,420** | | | 147 |
| **JUMLA KUU - G01** | | | **6,559,460,000** | | | **6,033,244,480** | | | **92** |
| | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki | 4,982,400,000 | 4,564,400,000 | **9,546,800,000** | 5,386,745,250 | 1,299,098,070 | **6,685,843,320** | 108 | 28 | 70 |
| Ruzuku ya Mahkama ya Kadhi | 930,900,000 | 335,900,000 | **1,266,800,000** | 954,446,493 | 95,800,000 | **1,050,246,493** | 103 | 29 | 83 |
| **Jumla ya Programu -G02** | | | **10,813,600,000** | | | **7,736,089,813** | | | **72** |
| | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Serikali** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Serikali | 1,545,932,000 | 1,649,368,000 | **3,195,300,000** | 1,348,493,355 | 999,798,800 | **2,348,292,155** | 87 | 61 | 73 |
| **Jumla ya Programu -G03** | | | **3,195,300,000** | | | **2,348,292,155** | | | **73** |
| | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai | 1,964,000,000 | 1,333,900,000 | **3,297,900,000** | 1,865,343,636 | 450,891,200 | **2,316,234,836** | 95 | 34 | 70 |
| Ruzuku ya Kituo cha Sheria | | 211,500,000 | | | 132,000,000 | 132,000,000 | | 62 | |
| **Jumla ya Programu - G04** | | | **3,297,900,000** | | | **2,448,234,836** | | | 74 |
| | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Mapitio ya Sheria | 602,700,000 | 1,299,090,000 | **1,901,790,000** | 607,987,180 | 325,643,800 | **933,630,980** | 101 | 25 | 49 |
| **Jumla ya Programu - G05** | | | **1,901,790,000** | | | **933,630,980** | | | **49** |
| | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini** | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Uendeshaji na Usimamizi wa Wakfu, Mirathi, Hijja, Zakka | 624,500,000 | 685,250,000 | **1,309,750,000** | 917,464,910 | 251,645,910 | **1,169,110,820** | 147 | 37 | 89 |
| **Jumla ya Programu - G12** | | | **1,309,750,000** | | | **1,169,110,820** | | | 89 |
| | | | | | | | | | |
| **Programu ya Huduma za Serikali Mtandao** | | | | | | | | | |
| Huduma za Serikali Mtandao | 1,503,555,000 | 2,800,445,00 0 | **4,304,000,000** | 871,487,825 | 788,624,800 | **1,660,112,625** | 58 | 28 | 39 |
| **Jumla ya Programu - G13** | | | **4,304,000,000** | | | **1,660,112,625** | | | **39** |
| | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini** | | | | | | | | | |
| Usimamizi na Utaratibu wa Taasisi na Masula ya Kiislamu | 639,600,000 | 902,600,000 | **1,542,200,000** | 698,513,350 | 251,577,300 | **950,090,650** | 109 | 28 | 62 |
| **Jumla ya Programu - G14** | | | **1,542,200,000** | | | **950,090,650** | | | **62** |
| | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi ya Maadili ya Viongozi wa Umma** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Maadili ya Viongozi wa Umma | 257,400,000 | 1,080,040,00 0 | **1,337,800,000** | 446,294,325 | 433,748,000 | **880,042,325** | 173 | 40 | 66 |
| **Jumla ya Programu - G15** | | | **1,337,800,000** | | | **880,042,325** | | | **66** |
| | | | | | | | | | |
| **Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma** | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma | 2,256,400,000 | 2,544,700,000 | **4,801,100,000** | 2,189,865,630 | 776,122,600 | **2,965,988,230** | 97 | 23 | 62 |
| **Jumla ya Programu -E04** | | | **4,801,100,000** | | | **2,965,988,230** | | | **62** |
| | | | | | | | | | |
| **Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi** | | | | | | | | | |
| Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi | 3,000,000,000 | 1,544,600,000 | **4,544,600,000** | 2,281,319,700 | 595,973,600 | **2,877,293,300** | 76 | 39 | 63 |
| **Jumla ya Programu -E05** | | | **4,544,600,000** | | | **2,877,293,300** | | | **63** |
| | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Watumishi wa Umma | 552,800,000 | 894,500,000 | **1,447,300,000** | 554,910,110 | 300,427,600 | **855,337,710** | 100 | 34 | 59 |
| **Jumla ya Programu -E07** | | | **1,447,300,000** | | | **855,337,710** | | | **59** |
| | | | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Watumishi Serikalini** | | | | | | | | | |
| Usimamizi wa Watumishi wa Umma | 209,590,000 | 511,300,000 | **720,890,000** | 251,341,200 | 128,102,400 | **379,443,600** | 120 | 25 | 53 |
| **Jumla ya Programu -E08** | | | **720,890,000** | | | **379,443,600** | | | **53** |
| **JUMLA KUU** | | | **45,775,690,000** | **22,595,628,734** | **8,641,282,790** | **31,236,911,524** | | | **68** |

**Kiambatanisho namba 1b: Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai/ Machi 2022/2023**

| **MAPITIO 2022/2023** | | | | **MUELEKEO 2023/2024** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **JINA LA MRADI** | **MCHANGO WA SERIKALI** | **MCHANGO WA WAHISANI** | **JUMLA** | **ASILIMIA** | **MCHANGO WA SERIKALI** | **MCHANGO WA WAHISANI JUMLA** | **JUMLA** |
| Mradi wa Uwezeshaji wa Upatikanaji wa Haki (LEAP) | | | | | | 969,631,552 | **969,631,552** |
| Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma (ZPSRP II) | 528,155,000 | 143,050,000 | **671,205,000** | | 750,000,000 | | **750,000,000** |
| Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria | 1,152,000,000 | | **1,152,000,000** | | 250,000,000 | | **250,000,000** |
| Mradi wa Upatikanaji wa Haki kwa Wanawake katika Kesi za Udhalilishaji (Gender Resposive Access to Justice respond cases against women and Children) | | | | | | 373,600,000 | **373,600,000** |
| Mradi wa Kujenga Uwezo wa Viongozi | 230,000,000 | | **230,000,000** | | | | |
| Mradi wa Kurahisisha Upatikanaji wa Huduma katikaUtumishi wa Umma | 86,950,000 | | **86,950,000** | | | | |

| MAKUSANYO 1c | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kiambatanisho Nambari 1c:Makusanyo ya Mapato Julai/ Machi 2022/2023 na Makadirio ya Mwaka 2023/2024** | | | | |
| | **Makusanyo ya Mapato Julai/ Machi 2022/2024** | | | **Makadirio ya Mwaka 2023/2024** |
| **IDARA/TAASISI** | **Makadirio** | **Makusanyo** | **Asilimia** | |
| Mahkama | 958,552,395 | 803,591,586 | 84 | 1,576,000,000 |
| **Jumla** | **958,552,395** | **803,591,586** | | **1,576,000,000** |
| Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali | 250,000,000 | 60,744,000 | 24 | 325,000,000 |
| **Jumla** | **250,000,000** | **60,744,000** | | **325,000,000** |
| Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana | 220,000,000 | 131,082,610 | 60 | 220,000,000 |
| **Jumla** | **220,000,000** | **131,082,610** | | **220,000,000** |
| Chuo Cha Utawala wa Umma | 1,630,876,000 | 1,304,869,500 | 80 | 2,035,900,000 |
| **Jumla** | **1,630,876,000** | **1,304,869,500** | | **2,035,900,000** |
| Skuli ya Sheria Zanzibar | 379,000,000 | 44,128,000 | 11 | 379,000,000 |
| **Jumla** | **379,000,000** | **44,128,000** | | **379,000,000** |
| **JUMLA KUU** | **3,438,428,395** | **2,344,415,696** | | **4,535,900,000** |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MUELEKEO** | | | | | | | |
| **Kiambatanisho nambari 2: Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024** | | | | | | | |
| **KAZI ZA KAWAIDA** | | | | **KAZI ZA MAENDELEO** | | | |
| **PROGRAMU KUU/ PROGRAMU NDOGO** | **MISHAHARA** | **MATUMIZI YA JUMLA** | **JUMLA** | **SMZ** | **WAHISANI** | **JUMLA** | **JUMLA KUU** |
| **Programu ya Masula ya Kisheria** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Masuala ya Kisheria | 108,333,200 | 115,000,000 | 223,333,200 | | | | |
| **Jumla ya Programu** | **108,333,200** | **115,000,000** | **223,333,200** | | | | |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utawala Bora | 216,566,320 | 100,000,000 | 316,566,320 | | | | |
| **Jumla ya Programu** | **216,566,320** | **100,000,000** | **316,566,320** | | | | |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Uendshaji na Uratibu wa ORKSUUB** | | | | | | | |
| Uendeshaji na Utawala | 1,645,301,480 | 1,100,000,000 | 2,745,301,480 | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mipango,Sera na Utafiti | 189,462,960 | 150,000,000 | 339,462,960 | 1,000,000,000 | 1,343,231,552 | | **2,343,231,552** |
| Uratibu wa ORKSUUB-Pemba | 336,024,020 | 174,000,000 | 510,024,020 | | | | |
| **Jumla ya Programu** | **2,170,788,460** | **1,424,000,000** | **3,594,788,460** | | | | |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Uendelezaji wa Utumishi wa Umma** | | | | | | | |
| Mipango na Maendeleo ya Watumishi | 300,000,000 | 335,667,400 | 635,667,400 | | | | |
| Miundo na Mifumo ya Taasisi | 193,700,000 | 519,344,620 | 713,044,620 | | | | |
| **Jumla ya Programu** | **493,700,000** | **855,012,020** | **1,348,712,020** | | | | |
| **Jumla ya Programu - G01** | **2,989,387,980** | **2,494,012,020** | **5,483,400,000** | **1,000,000,000** | **1,343,231,552** | | **7,826,631,552** |
| **Ruzuku G01** | | | | | | | |
| Chuo Cha Utawala wa Umma | 2,386,900,000 | | 2,386,900,000 | | | | |
| Skuli ya Sheria | | 370,600,000 | 370,600,000 | | | | |
| **Jumla ya Ruzuku - G01** | **2,386,900,000** | **370,600,000** | **2,757,500,000** | | | | |
| **JUMLA KUU - G01** | **5,376,287,980** | **2,864,612,020** | **8,240,900,000** | **1,000,000,000** | **1,343,231,552** | | **10,584,131,552** |
| | | | | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki | 7,462,900,000 | 3,767,600,000 | 11,230,500,000 | 27,000,000,000 | | | 38,230,500,000 |
| Ruzuku ya Mahkama ya Kadhi | 1,461,800,000 | 219,200,000 | 1,681,000,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - G02** | **8,924,700,000** | **3,986,800,000** | **12,911,500,000** | **27,000,000,000** | | | **39,911,500,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Serikali** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Serikali | 2,379,400,000 | 988,800,000 | 3,368,200,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - G03** | **2,379,400,000** | **988,800,000** | **3,368,200,000** | | | | **3,368,200,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai | 2,621,300,000 | 1,000,400,000 | **3,625,300,000** | | | | |
| Ruzuku ya Kituo cha Sheria | | 158,700,000 | **158,700,000** | | | | |
| **Jumla ya Programu -** | | | | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **G04** | **2,621,300,000** | **1,159,100,000** | **3,780,400,000** | | | | **3,784,000,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Mapitio ya Sheria | 827,400,000 | 1,039,300,000 | 1,866,700,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - G05** | **827,400,000** | **1,039,300,000** | **1,866,700,000** | | | | **1,866,700,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Haki na Uwezeshaji Kishariah** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Haki na Uwezeshaji Kishariah | 1,347,600,000 | 582,500,000 | 1,930,100,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - G12** | **1,347,600,000** | **582,500,000** | **1,930,100,000** | | | | **1,930,100,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Huduma za Serikali Mtandao** | | | | | | | |
| Huduma za Serikali Mtandao | 1,249,700,000 | 1,958,900,000 | 3,208,600,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - G13** | **1,249,700,000** | **1,958,900,000** | **3,208,600,000** | | | | **3,208,600,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini** | | | | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Usimamizi na Utaratibu wa Taasisi na Masula ya Kiislamu | 1,347,600,000 | 582,500,000 | 1,930,100,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - G14** | **1,347,600,000** | **582,500,000** | **1,930,100,000** | | | | **1,930,100,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi ya Maadili ya Viongozi wa Umma** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Maadili ya Viongozi wa Umma | 640,800,000 | 660,300,000 | 1,301,100,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - G15** | **640,800,000** | **660,300,000** | **1,301,100,000** | | | | **1,301,100,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma** | | | | | | | |
| Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma | 4,483,900,000 | 1,808,500,000 | 6,292,400,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - E04** | **4,483,900,000** | **1,808,500,000** | **6,292,400,000** | | | | **6,292,400,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi** | | | | | | | |
| Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma | 3,136,200,000 | 1,158,400,000 | 4,294,600,000 | | | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumla ya Programu - E05** | **3,136,200,000** | **1,158,400,000** | **4,294,600,000** | | | | **4,294,600,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Watumishi wa Umma | 520,900,000 | 728,000,000 | 1,248,900,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - E07** | **520,900,000** | **728,000,000** | **1,248,900,000** | | | | **1,248,900,000** |
| | | | | | | | |
| **Programu ya Usimamizi wa Watumishi Serikalini** | | | | | | | |
| Usimamizi wa Watumishi wa Umma | 458,600,000 | 409,100,000 | 867,700,000 | | | | |
| **Jumla ya Programu - E08** | **458,600,000** | **409,100,000** | **867,700,000** | | | | **867,700,000** |
| **JUMLA KUU** | **33,314,387,980** | **17,926,812,020** | **51,241,200,000** | **28,000,000,000** | **1,343,231,552** | | **80,584,431,552** |

**Kiambatanisho nambari 3 :TAKWIMU ZA MAHKAMA ZOTE UNGUJA NA PEMBA JULAI 2021 HADI JUNI 2022**

| MAHKAMA | JINAI | | | MADAI | | | RUFAA ZA JINAI | | | RUFAA ZA MADAI | | | MAOMBI YA JINAI | | | MAOMBI YA MADAI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla ya kesi zilizofunguliwa | Zilizotolewa uwamuzi | Zinazoendelea | Jumla ya kesi zilizofunguliwa | Zilizotolewa uwamuzi | Zinazoendelea | Jumla ya kesi zilizofunguliwa | Zilizotolewa uwamuzi | Zinazoendelea | Jumla ya kesi zilizofunguliwa | Zilizotolewa uwamuzi | Zinazoendelea | Jumla ya kesi zilizofunguliwa | Zilizotolewa uwamuzi | Zinazoendelea | Jumla ya kesi zilizofunguliwa | Zilizotolewa uwamuzi | Zinazoendelea |
| MAHKAMA UNGUJA | 9,465 | 8,460 | 1,005 | 1,749 | 876 | 873 | 55 | 2 | 53 | 91 | 17 | 74 | 124 | 59 | 65 | 104 | 11 | 93 |
| MAHKAMA PEMBA | 1,299 | 1,078 | 221 | 469 | 351 | 118 | 18 | 4 | 14 | 40 | 22 | 18 | 34 | 29 | 5 | 23 | 8 | 15 |

**Kiambatanisho nambari 4: MATANGAZO YA KISHERIA**

| NAM. | |
|---|---|
| 1. | Appointment of the Inspectors |
| 2. | Tangaazo la Majina ya Viongozi wa Umma |
| 3. | Notice of Intent to Create Forest Reserve |
| 4. | The Zanzibar Presidential Delivery Bureau Order, 2022 |
| 5. | Appointment of Assessors. |
| 6. | Extension of Jurisdiction for Rm. |
| 7. | Appointment of Judges of the Commercial Court |
| 8. | Amendment of the First Schedule of Import and Export of Precious Metals and Precious Stones |
| 9. | Appointment of State Attorneys |
| 10. | Appointment of the Government Analysts |
| 11. | Shahada ya Kuwasilisha Mswada wa Dharura |
| 12. | Appointment of State Attorney |
| 13. | Appointment of the Chairperson of the Board of the Commission for Land |
| 14. | Appointment of the Chairman of the Board of Director of Zanzibar Airport Authority |
| 15. | Appointment of the Chairman of the Roads Fund Board |
| 16. | Appointment of the Government Chief Pharmacist |
| 17. | Appointment of Director of Zanzibar Library Services |
| 18. | Appointment of Director of the Department of Administrative and Human Resources Management in the Ministry of Education and Vocational Training |
| 19. | Appointment of the Executive Secretary of the Commission for Land |
| 20. | Appointment of the Director General of the Medical Store Department |
| 21. | Appointment of the Executive Director of Zanzibar Economic Empowering Agency |
| 22. | Appointment of Treasury Registrar |
| 23. | Appointment of the Regional Administrative Secretaries |
| 24. | Appointment of the Managing Director of Zanzibar State Trading Cooperation |

| | |
|---|---|
| 25. | Appointment of the District Commissioner of Southern District Unguja |
| 26. | Appointment of Principal Secretary in the President's Office |
| 27. | Appointment of the Members of Zanzibar Planning Commission |
| 28. | Appointment of the Directors |
| 29. | Appointment of the Commissioner of Zanzibar Public Leader's Ethics Commission |
| 30. | Appointment of the Director General of Health in the Ministry of Health |
| 31. | Appointment of the Deputy Principal Secretaries |
| 32. | Declaration of the Compulsory Standard and the National Standard. |
| 33. | Corrigendum |
| 34. | Tangazo la Majina ya Viongozi wa Umma. |
| 35. | Appointment of the Government Analysts |
| 36. | Corrigendum |
| 37. | Declaration of the Compulsory Standard and the National Standard. |
| 38. | Designation of Scientific Authorities |
| 39. | Order for Amendment of the First Schedule the Excise Duty Act No.8 of 2017 |
| 40. | Appointment of the Deputy Vice Chancellor of the State University of Zanzibar |
| 41. | Appointment of the Chairperson of the Board of Director of the Public Procurement and Disposal of Public Assets Authority |
| 42. | Appointment of the Secretary of the Retire Second Vice President |
| 43. | Appointment of the Director of Department of Planning, Management and Human Resource in the Attorney General's Chamber |
| 44. | Appointment of the Regional Administrative Secretory of North Region Unguja |
| 45. | Appointment of the Personal Secretory to the Second Vice President |
| 46. | Appointment of the Officer In charge in the Ministry of Social Welfare, Elderly, Gender and Children |
| 47. | Uteuzi wa Makatibu Wakuu |
| 48. | Appointment of the Government Analysts |
| 49. | Declaration of the Compulsory and the National Standard |
| 50. | Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar |
| 51. | Appointment of the Government Chemistry |
| 52. | Uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wagurugenzi ya Wakala wa Uwekezaji Wananchi Kiuchumi |
| 53. | Appointment of the Executive Director of Mnazimoja Hospital |

**Kiabatanisho nambari 4b: KANUNI**

| NAM. | |
|---|---|
| 1. | The Stone Town Conservation and Development Authority (General Regulations), 2023 |
| 2. | Kanuni za Utumishi za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar,2023 |
| 3. | The Weight and Measure General Reguletions,2023 |
| 4. | The Zanzibar Drugs Control and Enforcement Authority Forms Regulations,2023 |
| 5. | The Zanzibar Bureau of Standards (Fees and Charges) Regulations,2022 |
| 6. | Kanuni za Tasisi za Viwango Zanzibar (Ada na Tozo) |
| 7. | Kanuni za Uendeshaji wa Vikao vya Baraza la Ulamaa na Uratibu wa Sherehe au Madhimisho ya Kislamu Zanzibar |
| 8. | The Tax Administration and Procedure Regulations, 2022 |
| 9. | Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar |
| 10. | The Business Licensing Administration (Amendment) Regulations,2022. |
| 11. | Kanuni za Usimamizi wa Vituo vya Mafuta.2022 |
| 12. | Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (Fao la Upotevu wa Ajira |

**Kimbatanisho nambari 4c**: **MISWADA YA SHERIA**

| NAM. | |
|---|---|
| 1. | Mswada wa Kufuta Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumi Uchumi Zanzibar |
| 2. | Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Mawasiliano Zanzibar |
| 3. | Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo cha Utawala wa Umma, 2022. |
| 4. | Mswada wa Sheria ya Kufuta sheria ya Watu Wenye Ulemavu na Kuandika Upya Sheria ya Watu Wenyeulemavu 2022. |
| 5. | Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, 2022. |
| 6. | Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar 2022. |
| 7. | Mswada wa Kufuta Sheria ya Bodi ya Mapato Zanzibar na Kuanzisha Mamlaka ya Mapato 2022. |
| 8. | Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, 2022. |

**Kiambatanisho nambari 5: Tuhuma za Rushwa kwa kipindi cha Julai/ Machi 2022/2023**

| TUHUMA | ZILIZOPOKELEWA | ZINAZOENDELEA NA UCHUNGUZI | ZILIZOFUNGWA | ZILIZOHAMISHIWA TAASISI NYINGINE | ZILIZOFANYIWA UDHIBITI | ZILIZOTOLEWA USHAURI | ZILIZOPELEKWA KWA DPP | ZILIZOPO MAHAKAMANI | ZILIZOTOLEWA HUKUMU | ZILIZOKUTWA NA HATIA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya jambo kinyume na ushindani wa soko | 1 | | | 1 | | | | | | |
| kughushi nyaraka | 7 | 5 | 1 | 1 | | | | | | |
| Kujipatia pesa kwa njia ya udanganyifu | 3 | 1 | | | 1 | 1 | 1 | | | |
| Kukwepa kulipa kodi | 11 | 6 | | 2 | 3 | | | | | |
| Kumdanganya muajiri | 1 | | | 1 | | | | | | |
| Kumkwaza Afisa wa ZAECA | 1 | | | | | 1 | | | | |
| Kusafirisha Magendo | 3 | 3 | | | | | 1 | | | |
| Kushawishi kuomba na kupokea rushwa | 15 | 9 | 1 | | 2 | 3 | 3 | 1 | | |
| Kutumia vibaya mali | 9 | 6 | | 1 | 1 | 1 | | | | |
| Matumizi mabaya ya Ofisi | 39 | 25 | 3 | 2 | 6 | 3 | | | | |
| Rushwa katika uwakala | 3 | 1 | 1 | | | 1 | | | | |
| Mirathi | 1 | | | 1 | | | | | | |
| Rushwa katika zabuni | 4 | 4 | | | | | | | | |
| Rushwa ya ngono | 2 | | 2 | | | | | | | |
| Ubadhirifu wa mali na mapato | 58 | 38 | 4 | 2 | 6 | 8 | 11 | | 1 | 1 |
| Uharibifu wa mali | 1 | | | | | 1 | | | | |
| Utapeli | 2 | | | | | 2 | | | | |
| **JUMLA NDOGO** | **161** | **98** | **12** | **11** | **19** | **21** | **16** | **1** | **1** | **1** |

**sho nambari 6a**: **WATUMISHI WALIOAJIRIWA KUANZIA JULAI, 2022 HADI KUFIKIA MACHI, 2023**

| WIZARA / TAASISI | | JUMLA |
|---|---|---|
| 1 | Wizara ya Afya | 777 |
| 2 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 1,327 |
| 3 | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | 17 |
| 4 | Wizara ya Fedha na Mipango | 3 |
| 5 | Ofisi ya Mufti mkuu Zanzibar | 4 |
| 6 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu | 9 |
| 7 | Tume ya Mipango | 2 |
| 8 | Tume ya Maadili ya Viongozi | 12 |
| 9 | Wakala wa Serikali mtandao | 6 |
| **JUMLA** | | **2,157** |

## Kiambatanisho nambari 6b: SHUGHULI ZA TUME YA UTUMISHI SERIKALINI KUANZIA JULAI, 2022 HADI KUFIKIA MACHI, 2023

| WIZARA/TAASISI- | KUTHIBITISHWA KAZINI | NYONGEZA YA MUDA WA UTUMISHI | UAJIRI WA MKATABA | KUSTAAFU KWA MARADHI | KUSTAAFU KWA LAZIMA | KUSTAAFU KWA HIARI | LIKIZO BILA YA MALIPO | KUBADILISHWA KADA | KUACHA KAZI | KUFUKUZWA KAZI | KUPANDISHWA DARAJA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 799 | 1 | 2 | 3 | 407 | 4 | 4 | 11 | | | 25 |
| Wizara ya Fedha na Mipango | 2 | - | - | - | - | - | - | 22 | | | 3 |
| Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo | 55 | - | - | - | - | - | - | 16 | - | - | 1 |
| Wizara ya Afya | 330 | - | 4 | 1 | 93 | - | 2 | 46 | | | 20 |
| Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora | 13 | - | - | - | - | - | - | 10 | - | - | - |
| Wizara Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi | 75 | 1 | | 1 | 84 | - | - | 15 | 1 | - | 2 |
| Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Ikulu na Mwenyekiti wa BLM | 24 | - | 7 | 1 | 2 | - | - | | - | - | - |
| Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais | 1 | - | - | - | 1 | - | - | 2 | - | 1 | 1 |
| Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais | 8 | - | - | - | 6 | - | - | 3 | | - | 8 |
| Tume ya Madawa ya Kulevya | | | 5 | - | - | - | - | | | | - |
| Wizara ya Mawasiliano | | | 11 | | | - | - | | | | - |
| Baraza la Mji Kaskazini A | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 2 |
| Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji | 1 | - | - | - | - | - | - | | - | - | - |
| Baraza la Mitihani | 5 | - | - | - | 1 | - | - | - | - | | - |
| Wizara ya Biashara na Maendeleo | - | - | - | - | 4 | - | - | 1 | - | - | - |
| Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu | - | - | - | - | 7 | - | - | | - | - | 1 |
| Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka | - | - | - | - | 1 | - | - | - | - | - | - |
| Ofis ya Mkemia Mkuu wa Serikali | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 1 |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Taasisi ya Viwango | - | - | 3 | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Chuo cha Kiislamu | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 1 |
| Tume ya Mipango | - | - | - | - | 2 | - | | - | - | - | - |
| Baraza la Manispaa Magh.B | 31 | - | - | - | - | - | - | 6 | - | - | 2 |
| Mamlaka ya Mafunzo ya Amali | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Baraza la Manispaa Mjini | 5 | - | - | 4 | - | - | - | 5 | - | - | - |
| Shirika la Huduma za Maktaba | | - | - | - | 3 | - | - | - | - | - | - |
| Mamlaka ya Ununuzi na uondoshaji wa mali za umma | - | - | - | - | 1 | - | - | - | - | - | - |
| Afisi ya Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | - | - | - | - | 1 | - | - | 19 | - | - | - |
| Shirika la nyumba | | | - | | 1 | | | - | | | |
| Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi | 16 | - | - | - | - | - | - | 5 | - | - | 2 |
| Baraza la Manispaa Magh.A | | | - | - | | - | - | 5 | - | - | 1 |
| Ofisi ya Mwanasheria Mkuu | | | - | - | 4 | - | - | - | | | - |
| Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja | 21 | - | - | - | - | - | - | 3 | - | - | 1 |
| Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja | | | - | 1 | | - | - | 1 | - | - | 1 |
| OR Kazi Uchumi na Uwekezaji | - | - | - | - | 22 | - | - | 19 | - | - | 1 |
| Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba | 18 | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Baraza la Jiji | 7 | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 1 |
| Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba | | | - | - | 5 | - | - | - | | | - |
| Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ] | - | | - | - | 12 | - | - | 3 | - | - | 2 |
| Mamlaka ya Hifadhi ya Mji Mkongwe | - | - | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - |
| Shirika la Huduma za Maktaba | | - | - | - | 4 | - | - | 2 | - | - | - |
| Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | | - | - | 1 | 5 | - | - | 2 | - | - | - |
| Taasisi ya Elimu | 1 | - | - | - | | - | - | - | - | - | - |
| Wakala wa Barabara | 3 | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar | 3 | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | - |
| Hospitali ya Rufaa Mnazi Mmoja | 4 | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | 4 |

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Baraza la Mji Kati | 53 | - | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - |
| Ofisi ya Wakfu na Mali ya Amana | - | - | - | - | 1 | - | - | - | - | - | - |
| Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira | 1 | - | - | - | 8 | - | - | 1 | - | - | 3 |
| Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale | 3 | - | - | - | 6 | - | - | 1 | - | - | 2 |
| Wizara ya Maji na Nishati | 1 | - | - | - | - | - | - | 5 | - | - | 1 |
| Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ | 10 | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Wizara ya Maendeleo ya Jamii | 11 | - | - | - | 5 | - | - | 9 | - | - | - |
| Baraza la Mji Mkoani | 40 | - | - | - | 3 | - | - | 2 | - | - | - |
| Tume ya Uchaguzi | | | - | - | 1 | - | - | | | | - |
| Mamlaka ya Mapato Zanzibar | | | 121 | - | | - | - | | | | - |
| Tume ya Maadili ya Viongozi | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - | 1 |
| Tume ya Utumishi Serikalini | - | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - | - |
| Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa kiuchumi | 4 | - | - | - | - | - | - | 1 | - | - | 2 |
| Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja | 5 | - | - | - | - | - | - | 2 | - | - | - |
| Kamisheni ya Utumishi wa Umma | - | - | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - |
| Baraza la Mji Chake Chake | 21 | - | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Wakala wa Serikalini Mtandao | - | - | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - |
| Baraza la Mji Wete | - | - | - | - | 24 | - | - | 1 | - | - | - |
| **JUMLA KUU** | **1571** | **2** | **153** | **12** | **714** | **4** | **7** | **226** | **1** | **1** | **89** |

**Kiambatanisho nambari 6c: MALALAMIKO YA WAFANYAKAZI JULAI - MACHI 2022/2023**

| Nam | WIZARA / TAASISI | IDADI YA WATUMISHI | AINA YA LALAMIKO LINALOWASILISHWA | UAMUZI ULIOFIKIWA NA TUME |
|---|---|---|---|---|
| | | W'ME | | |
| 1 | Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango | 1 | Kupatiwa stahiki zake | Dai limekubaliwa na muhusika amepatiwa haki zake |
| 2 | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, IdaraMaalum za SMZ | 1 | Kuhusiana na Ajira na Haki zake | Dai limeshughulikiwa na muhusika amepatiwa haki zake. |
| 3 | Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango | 1 | Kushushwa Cheo | Dai limeshughulikiwa na kufanyiwa kazi |
| | **JUMLA** | **3** | | |